**WANANCHI** Bagamoyo wafunguka kuhusu fursa ujenzi wa bandari

UKURASA 4



**MKATABA** wa biashara Afrika sasa kuinufaisha Tanzania usafirishaji bidhaa bila vikwazo

UKURASA 3




UKURASA 11


# Nipashe

MWANGA WA JAMII

Jumanne Juni 29, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580626

www.ippmedia.com

The Guardian digital · nipasheTZ · nipasheTZ · nipasheTZ · 0745 700710


# SAMIA ATOA MWELEKEO

**NI** Katiba mpya, takwimu za corona, ripoti ya uchunguzi BoT, mkutano wa kisiasa...

*Endelea Ukurasa wa 2*




Rais Samia Suluhu Hassan, akizungumza na wahariri wa vyombo vya habari (hawapo pichani) kuhusu siku 100 tangu kuingia madarakani katika ukumbi wa Jakaya Kikwete Ikulu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

## YALIYOMO

UKURASA WA 4

### PAC YATAKA KAMATI UFUATILIAJI

MWENYEKITI wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), Naghenjwa Kaboyoka, amelishauri Bunge kuunda Kamati ya Ufuatiliaji...

UKURASA WA 4

### KAMPUNI YA ULINZI YAONYWA WIZI BENKI

JESHI la Magereza limewaagiza askari wa Kampuni ya Ulinzi ya Shima Guard, waliohitimu mafunzo ya uaskari kuacha kushawishiwa kuiba katika benki ikiwamo kuwaibia...

UKURASA WA 5

### MPANGO KUMWAKILISHA SAMIA KONGAMANO KIZAZI CHA USAWA

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, anatarajia kumwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan, katika...

## Kishindo cha Mdude siku 414 gerezani

UKURASA 3




Waziri wa Madini, Dotto Biteko (kushoto), akishangilia na wafanyakazi wa Benki ya NMB baada ya kuzindua rasmi Klabu ya Madini jijini Dodoma jana. NMB imeanzisha klabu hizo kwa lengo la kuwawezesha mikopo wachimbaji na wafanyabiashara wa madini nchini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## BUNGE LAJITOSA KWENYE KANUNI UANZISHWAJI WA BODI YA WALIMU

UKURASA 3

**MICHEZO** **GOMES, NABI WALIAMSHA MTIFUANO SIMBA, YANGA** UK. 24

**MAONI, KATUNI UK. 6**

HABARI KITAIFA

# Rais ataka subira Katiba mpya, mikutano vyama vya kisiasa

**Na Christina Mwakangale**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amesema Watanzania wasubiri hatua ya serikali kuruhusu mikutano ya hadhara ya kisiasa pamoja na upatikanaji wa Katiba mpya, akisema nchi ijenge uchumi kwanza.

Amesema Tanzania kama nchi nyingine inapitia changamoto ya kudorora kwa uchumi na kwamba mwaka jana uliporomoka hadi asilimia nne ingawa mwaka huu umepanda na kufikia tano.

Rais Samia aliyasema hayo jana, Ikulu, jijini Dar es Salaam, wakati akizungumza wahariri na waandishi kutoka katika vyombo mbalimbali vya habari nchini kuhusu siku 100 tangu alipoingia madarakani.

"Naomba Watanzania wawe na subira. Nimeshapanga kukutana na wanasiasa na kuhusu Katiba mpya, vyote vitashughulikiwa. Ila kuna yaliyo kipaumbele kwanza kwa nchi, ikiwamo uchumi... kila kitu kitakaa sawa uchumi ukiimarika. Tayari wawekezaji waliosajiliwa ni mara mbili kuliko mwaka jana. Hii itakuza uchumi na mapato pamoja na ajira.

"Nimeanza kukutana na wenzangu, watafuata wengine ila nipewe muda kusimamisha nchi kiuchumi, itafuata kushughulikia katiba mpya na kuruhusu mikutano ya hadhara. Katiba ni ya maana sana, msubiri nisimamishe nchi kiuchumi, tutakwenda katika siasa."

Rais Samia alisema pamoja na mikutano ya hadhara kutoruhusiwa, bado vyama vya siasa vinaendelea na mikutano yao kwenye maeneo yao ikiwamo majimbo kwa kufanya mikutano ya ndani.

Aidha Rais Samia alisema pamoja na kazi ya urais kuwa ngumu kutokana na mazingira alivyopokea kiti hicho, kufuatia kifo cha Hayati Dk. John Magufuli, bado anapata matumaini na moyo kila anapokutana na taasisi mbalimbali na makundi.

"Urais unakuwa rahisi kama umejiandaa kuwa rais, kuichukua nchi unakuwa umeshajipanga kwa kampeni na kukabili, nilizunguka ndio na kupiga kampeni, nikajua nina bonge la kaka atachukua, ule mzigo... sasa mzigo umekuja mabegani kwangu, sikupata uzito sana sababu nilijua tulichojipanga, tulikuwa pamoja. Ila ni kazi ngumu.

"Ingawa nathibitisha naweza kwenda nalo, kwa ushirikiano na kwa kuwa urais ni taasisi pia ushirikiano upo kutoka kwenu vyombo vya habari.

"Pamoja na kazi ya urais kuwa ngumu inakuwa rahisi kwa kuwa ninakutana na taasisi hata vyombo vya habari. Kwa siku moja faili zinaingia 20 hadi 30, uzifanyie kazi siku moja kwa maelekezo, au wewe mwenyewe," alisema Rais Samia.

**UCHUNGUZI BOT**

Kuhusu ripoti ya uchunguzi katika Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kwa miezi mitatu kuanzia Januari hadi Machi mwaka huu kama alivyomwagiza Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Rais Samia alisema uchunguzi huo umekamilika kwamba anatarajia kuitoa kesho.




Mwanazuoni wa Shule Kuu ya Sheria, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Prof. Khoti Kamanga (katikati), akizungumza kwenye mkutano uliohusisha wadau wa haki za binadamu na kusaidia wakimbizi, mwishoni mwa wiki kwenye maadhimisho ya Siku ya Wakimbizi Duniani. PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE

# ... Asema watu 100 wanaugua corona

**Na Christina Mwakangale**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amesema Tanzania kuna wagonjwa takribani 100 wanaougua ugonjwa wa Covid-19, na kwamba kati yao wanatumia oksijeni.

Amesema kwa kuwa Tanzania sio kisiwa, kuna haja ya kuungana na nchi nyingine duniani katika mapambano ya corona ikiwamo kutoa chanjo kwa wananchi na kwamba serikali imetenga Dola milioni 479 kwa ajili ya kujipanga kuagiza chanjo na vifaa.

Rais Samia aliyasema hayo jana, Ikulu, jijini Dar es Salaam, wakati akizungumza na wahariri na waandishi kutoka katika vyombo mbalimbali vya habari nchini.

"Nusu ya fedha hizo zitatumika kwa ajili ya kuagiza chanjo. Sasa tumeamua twende kama dunia inavyokwenda, wimbi la kwanza halikuathiri sana, la pili liliathiri pakubwa. Na la tatu tayari tuna wagonjwa, tuna wagonjwa 100 zaidi kati yao 70 wapo katika matibabu ya oksijeni taarifa hii ni hadi juzi," alisema Rais Samia.

"Tuchanjwe kwa hiari, mtu kwa nafsi aisikilize nafsi yake kuna Watanzania ambao wameshachanjwa nje ya nchi wanafanya shughuli zao nchi kama kawaida. Tunaruhusu jumuiya za kimataifa kupokea chanjo zipokewe ziletwe."

Alisema kuwapo kwa corona Tanzania kama nchi nyingine inapitia changamoto ya kudorora kwa uchumi, na kwamba alipoingia madarakani alichukua hatua kadhaa ikiwamo kuunda kamati kwa ajili ya suala hilo.

"Nilipoingia madarakani nilitamani tushughulikie kama nchi nyingine na ukubwa wake, nikaunda kamati kwa kazi ya wiki tatu na ripoti ya kwanza ikaletwa na kuwaambia kitaalumа tutashughulikia vipi.

"Chanjo ipi, namna ya kuzitunza, ni zipi tuwe nazo. Tiba ya asili zinazofanya kazi kupitia bodi inayofanyia uchunguzi kitaalamu zitatumika kama tiba mbadala. Zilizokidhi vigezo zitumike. Zinachangia pakubwa," alisema na kuendelea:

"Hivi karibuni niliangalia makala fulani ya nje ya nchi, kuhusu kujifukiza kabla wadudu hawajafika kichwani wanaondoka, kabla ya kushuka kifuani, ni vitunguu tu na vicks, kwa siku tatu corona imeondoka, tunajifunza kutoka kwa wengine. Kuna jumuiya za kichina hapa nchini wameomba chanjo zao zichanjwe. Nikajiuliza kwa hali nchi yetu ya kiuchumi tunafanyaje fedha tunatoa wapi."

Alisema Tanzania iliwahi kutuma maombi katika mpango wa COVAX facility ambao ni maalumu kwa nchi zenye uchumi wa chini, kuingia katika mradi huo, ambao hadi Juni 15, mwaka huu ulikuwa mwisho wa kutuma maombi ya kupata chanjo kutoka mpango huo.

"Mpango wa COVAX ulikuwa mwisho kama hujasema unataka, itakubidi usubirie ili upate chanjo hadi mwaka 2023, nikasema tujiunge, kuagiza na kuchanja itafuata. Tunaweza tukawa na watakaolipia na kuchanjwa na nyingine kwa ajili ya wananchi kuchanjwa.

"Ila wataalamu wa afya watuambua ni chanjo ipi. Hatujapuuza hili. Kupambana na corona si serikali pekee bali na wananchi kwa kuchukua tahadhari, kama wanaoamini kwa kufukiza sawa na uvaaji wa barakoa, kunawa mikono uzingatiwe, kupunguza maambukizi.

## Vyombo habari vilivyofungiwa kupata leseni

**Na Christina Mwakangale**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amesema vyombo vya habari ambavyo vilipewa adhabu mbalimbali na kufungiwa virudi Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa ajili ya kupatiwa leseni upya.

Aidha, amesema malalamiko kutoka kwa vyombo vya habari hususani vya binafsi kutopatiwa matangazo kutoka serikalini, amesema utumike ushindani uliowekwa katika kupata matangazo hayo.

Alikuwa akijibu baadhi ya maswali kutoka kwa Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), Deodatus Balile, kuhusu serikali itakavyochukua hatua kunusuru vyombo vya habari baada ya wimbi la corona na kufanya baadhi kushindwa kujiendesha na kufungwa.

Kadhalika, rais alijibu maswali mengine kutoka kwa wahariri na waandishi wa vyombo hivyo, kuhusu sekta mbalimbali ikiwamo ushirikishwaji wao kwenye mipango ya maendeleo ya kitaifa.

Rais Samia alisema vyombo vya habari vina mchango mkubwa kwa nchi ikiwamo kulinda usalama wa nchi, na kufichua uovu ambao ukifichuliwa serikali huchukua hatua.

Alisema amepata ushirikiano kutoka vyombo vya habari tangu aingie kuongoza nchi katika kipindi cha siku 100 , na kwamba serikali itaendelea kutoa ushirikiano wa kutosha kwa vyombo vyote.

"Niwahakikishie wakati wangu huu sitakataza kupata matangazo, bali itakuwa ushindani katika kuyapata. Madeni mliyoyasema tutayapitia na kuthibitisha kama halali na kuanza kulipa kwa awamu," alisema.

Kuhusu Baraza la Habari, kupata ruzuku ili kuendesha shughuli zakee kama ilivyo Mahakama na Bunge, alisema suala hilo ni la Katiba ingawa linazungumzika ili kutatua tatizo.

"Vyombo vyote vya habari sasa vitaingia katika mipango ya maendeeo ya taifa. Ada na leseni kulipwa kwa dola tutaangalia."

"Miradi mikubwa niwahakikishie bwawa la Nyerere itakwenda vizuri kupitia bajeti hii, miradi kadhaa ya umeme, maji vijijini, itafanyika kama tulivyopanga.

"Magazeti yaliyomaliza kifungo yaombe leseni upya na kuendelea na kazi lakini kwa kufuata sheria," alisema huku akitaka heshima na sheria ichukue mkondo wake, na kwamba serikali ikosolewe na kuonyeshwa njia. Balile alisema licha ya matangazo hayo kutolewa na vyombo hivyo lakini hayalipwi kwa wakati na sasa yamefikia Sh. bilioni 6.5 hadi bilioni 6.8 ambayo kampuni nane zinaidai serikali. Alisema janga la corona kwa nchi nyingine zimetumika ruzuku ili kuviinua vyombo vya habari ambavyo vimekumbwa na tatizo la kiuchumi kipindi cha Covid-19.

"Kuna vyombo vya kisheria katika taaluma kadhaa, kama mkandarasi, madaktari na wanasheria. Baraza la Habari Tanzania (MCT) halina fedha za kujiendesha kutoka serikalini. Hatushirikishwi mipango ya kitaifa ya maendeleo tunaomba tushirikishwe," alisema Balile.

## HABARI KITAIFA

# Kishindo cha Mdude siku 414 gerezani



Mwanaharakati na kada wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Mdude Nyagali (katikati mwenye tisheti nyekundu) akishangilia pamoja na wafuasi wengine wa chama hicho jana, baada ya Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Mbeya kumwachia huru katika kesi iliyokuwa inamkabili ya usafirishaji wa dawa za kulevya. **PICHA: NEBART MSOKWA.**

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

BAADA ya Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Mbeya, kumwachia huru mwanaharakati na kada wa CHADEMA, Mdude Nyagali, amewashukuru wanachama wa chama hicho waliokuwa wanamhudumia kwa siku 414 alizokuwa gerezani.

Nyagali aliachiwa huru jana baada ya kutuhumiwa kwa kosa la kukutwa na dawa za kulevya aina ya heroine gramu 23.4.

Akizungumza na wanachama wa CHADEMA kwenye ofisi za chama hicho Kanda ya Nyasa, Mdude alimshukuru Mungu kwa kumsaidia kwenye kesi hiyo akisema kuwa Mungu ni mkubwa kuliko madikteta wote duniani hata wakiungana.

Alisema kuachiliwa huru kwake na mahakama hiyo ni tafsiri tosha kwamba mahakama zimeanza kuwa huru na zinafanya kazi kwa kuzingatia misingi ya haki.

"Leo ni siku ya kufurahia haki hii, lakini mtapewa taarifa siku ambayo tutakutana ili niteme nyongo, nawashukuru kwa kuungana nami katika siku zote 414 ambazo nilikuwa gerezani, mmenichangia fedha za kujikimu na mmemchangia wakili wangu, nawashukuru sana," alisema Mdude.

Katibu wa CHADEMA Kanda ya Nyasa, Emmanuel Masonga, alisema baada ya Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Mbeya kumwachilia huru Mdude, wanakusudia kuendelea kuwapigania wanachama wengine wa chama hicho walioko magerezani.

Alisema katika Mkoa wa Songwe kuna wanachama wengine 40 ambao alidai wamewekwa magerezani kwa makosa ya kubambikiwa, kwamba harakati hizo zitafanyika nchi nzima.

"Kuna vijana wetu tuliwatuma wamezunguka kwenye magereza nchi nzima na kujionea namna Watanzania walioko huko wanavyoteseka, sasa tutadai hii haki, katiba mpya, tume huru ya uchaguzi na uchaguzi huru," alisema Masonga.

HUKUMU YA KESI

Akisoma hukumu ya kesi hiyo namba 136 ya Mwaka 2020, Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Mbeya, Zawadi Laizer, alisema mahakama hiyo ilibaini upungufu mbalimbali kwenye ushahidi wa upande wa mashtaka.

Alisema mahakama hiyo ilibaini kuwa wakati Jeshi la Polisi linaenda kufanya upekuzi nyumbani kwa Mdude, funguo zilichukuliwa bila kufuata sheria na kwamba mashahidi walitoa ushahidi unaotofautiana kuhusu namna walivyozikuta dawa hizo.

Vilevile, alisema upekuzi uliofanywa nyumbani kwa Mdude haukuwa wa haki na wazi kutokana na mmoja wa maaskari waliokuwa wanafanya upekuzi huo kushtakiwa na mtuhumiwa kuwa alikuwa haungani nao kuingia kwenye kila chumba kufanya upekuzi.

Hakimu Laizer alisema maaskari waliofanya upekuzi nyumbani kwa Mdude walikiuka sheria kutokana na kufanya kazi hiyo bila kuwa na kibali kinachowaruhusu kufanya hivyo.

"Kwa mashaka hayo kuna uwezekano dawa hizo za kulevya ziliwekwa na Polisi nyumbani kwa Mdude Nyagali ama wakati wa upekuzi au kabla ya upekuzi, kwa hiyo kutokana na mashaka hayo mahakama inamwachia huru Mdude," alisema Laizer.

Wakili wa upande wa utetezi, Faraji Mangula alisema kitendo cha mahakama hiyo kutoa haki kwa Mdude ni tafsiri tosha kwamba serikali imekuwa ya haki.

Vilevile alisema mahakama imedhihirisha kuwa ni chombo huru ambacho kinatafsiri sheria.

NJE YA MAHAKAMA

Jana asubuhi, Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Mbeya, ilifurika wanachama na wafuasi wa CHADEMA nje na ndani ambao walikuwa wamevalia sare za chama hicho wakiwa na matumaini ya mwenzao huyo kuachiwa.

Hata hivyo, baada ya mahakama kumwachia huru, Mdude aliambatana na wanachama wenzake wa CHADEMA kuimba na kushangilia kutoka mahakamani mpaka zilipo ofisi za chama hicho za kanda.

## Mkataba biashara Afrika kuleta fursa

**Na Salome Kitomari**

SERIKALI imesema imekamilisha vifungu vyote muhimu kwenye mkataba wa biashara kwa nchi za Afrika, ambao utaruhusu wananchi kusafirisha mazao na bidhaa katika nchi hizo bila vikwazo.

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula, aliyasema hayo jana alivyokutana na Katibu Mtendaji wa Eneo huru la Biashara la Afrika (AfCFTA), Wamkele Mene, aliyekuja nchini kwa ajili ya kujitambulisha na kufahamiana na uongozi mpya wa nchi.

Akizungumza baada ya kujitambulisha Katibu Mkuu huyo, alisema ameridhishwa na hatua zinazochukuliwa na serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan, jambo lililoongeza nafasi yake ya uongozi Afrika.

"Sekretarieti inavutiwa na uamuzi wa serikali kushiriki tena kuchukua jukumu la uongozi ambalo limehusishwa tangu enzi za Rais Julius Nyerere, lengo ni kuonana na uongozi wa Tanzania na kushawishi umuhimu wa nchi kujiunga," alisema.

Alisema baaada ya ukoloni, bara sasa linafanya kazi kufungua na kuunganisha bara ili kuunda masoko na kuwezesha biashara na kwamba eneo hilo ni suluhisho la changamoto za maendeleo na kwamba Afrika ina uwezo wa kuiwezesha Afrika kukua kibiashara, kuboresha uchumi wa kiwango na kuanzisha soko jumuishi.

Naye Balozi Mulamula alisema mkataba huo ulisainiwa na nchi nyingine Machi mwaka 2018 na ulinza kutumika Mei 2019, na kwamba Tanzania haijachelewa kwa kuridhia mkataba huo sasa.

"Tanzania kuingia kwenye mkataba huu manufaa ni makubwa sana, tukiingia tuna uhakika wa soko kubwa la zaidi ya watu bilioni moja. Mchakato mzima wa kuridhia mkataba umefikia mwisho inayosubiriwa ni hatua ya mwisho ili turidhie na kusaini, hatutachukua muda mrefu," alisema.

# Bunge lajitosa Bodi ya Walimu

**Na Godfrey Mushi, DODOMA**

BUNGE limesema limebaini mchakato wa utungaji wa kanuni za uundwaji wa Bodi ya Kitaaluma ya Ualimu ya mwaka 2020 ulifanywa na serikali pasipo kuwashirikisha walimu.

Hivyo, limeitaka mamlaka inayohusika na kanuni hizo za bodi kuona haja ya kukaa na wadau wanaoguswa na kanuni, ili kupata mawazo jumuishi.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo, Ridhiwan Kikwete, wakati anawasilisha bungeni taarifa kuhusu uchambuzi wa sheria ndogo, alisema wamebaini wadau husika ambao ni Chama cha Walimu Tanzania (CWT) na mashirika yanayojihusisha na masuala mbalimbali ya walimu hawakushirikishwa.

"Jambo hilo limesababisha masuala muhimu yanayowahusu walimu kutowekwa katika kanuni au kuwekwa kwa namna inayoweza kuleta changamoto katika utekelezaji wake.

"Kamati imebaini kuwa mchakato wa kutengeneza Kanuni za Bodi ya Ualimu, 2020 ulihusisha mamlaka mbalimbali serikalini bila kuwashirikisha wadau waliotarajiwa kuguswa moja kwa moja na masharti ya kanuni hizo."

"Ushirikishaji wa wadau na hasa wale wanaoguswa moja kwa moja na sheria au kanuni inayotungwa, ni jambo linalozingatia umuhimu wa mtazamo wa wengi.

Kwa mujibu wa Ridhiwan, katika uchambuzi wao wamebainisha kuwa Kanuni ya 37 (1), inaruhusu kukata rufani dhidi ya uamuzi wa Bodi ya Walimu ndani ya siku 30, baada ya kutolewa kwa uamuzi, lakini masharti hayo ya kukata rufani yaliyowekwa na sheria ndogo, yanatofautiana na masharti yaliyoweka na Bunge katika sheria mama ambayo ni siku 90.

Aidha, sababu nyingine iliyosababisha Bunge, kutaka serikali kuwatafutia ahueni walimu katika kanuni hizo, ni masharti yanayopunguza siku za kukata rufani zilizoruhusiwa na Bunge.

Aidha Ridhiwan, alisema dosari hiyo inapunguza wigo wa haki uliotolewa na Bunge, jambo ambalo Bunge, haliwezi kuruhusu.

Baadhi ya wabunge waliochangia hoja hiyo ni Mwenyekiti wa Bunge, Najma Giga, Mbunge wa Moshi Mjini (CCM), Priscus Tarimo na Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Neema Lugakingira.


**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DAR ES SALAAM**
**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**MIRATHI Na. 74 YA MWAKA 2021**
**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU**
**HAROON DAWOOD ABDALLAH**
**MWOMBAJI/WAOMBAJI**
**ZAKARIA HAROON**
**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya Marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamisha kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa Mirathi kwa Waombaji/Mwombaji hapo juu. Mapingamizi yoyote kuhusu haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 14th Mwezi wa 7, 2021.

Imewasilishwa Dar es salaam, leo tarehe 24 Mwezi wa 6, 2021.

NAIBU MSAJILI

216334702

# Bagamoyo waeleza fursa ya bandari

**Na Julieth Mkireri,** BAGAMOYO

BAADHI ya wakazi wa Mji wa Bagamoyo mkoani Pwani wameeleza namna watakavyonufaika na ujenzi wa bandari ya Bagamoyo, ikiwamo kukua kwa uchumi na mji huo kupata hadhi.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo, Mohamed Usinga, alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuruhusu mazungumzo kuhusiana na mradi huo kuanza upya, ili ikiwezekana ujenzi wa bandari uanze mapema.

Usinga alisema endapo mradi huo utajengwa, moja ya faida zitakazopatikana ni pamoja na kukua kwa uchumi na ongezeko la uwekezaji katika sekta ya viwanda.

"Uwapo wa bandari utachochea kuwapo kwa viwanda vingi zaidi na vijana watapata ajira, tutaongeza pia idadi ya watu na maendeleo," alisema.

Alisema uwapo wa bandari hiyo utaiwezesha halmashauri kupata mapato ambayo yatatekeleza miradi ya maendeleo na asilimia 10 ya mikopo kwa makundi maalum ya wajasiriamali itapatikana.

Pia alieleza kuwa bandari itapanuliwa miundombinu katika mji huo wa kihistoria, barabara ya Bagamoyo - Dar es Salaam na ya Mlandizi (ya Makofia) itajengwa kwa kiwango cha lami na nyingine zinazoingia katika mji huo zitaboreshwa.

Mbunge wa Bagamoyo, Muharami Mkenge, alisema bandari hiyo ikijengwa itasaidia kuongeza ajira za moja kwa moja, na kwamba mradi huo hautakuwa faida wa Bagamoyo pekee, bali Taifa zima.

Alisema pia mradi utapunguza msongamano uliopo katika Bandari ya Dar es Salaam, kwa kuwa meli kubwa na za kati zitashusha mizigo Bagamoyo.

Mkenge alisema nchi nyingi zinategemea Bandari ya Dar es Salaam, hivyo foleni inapozidi siku hadi siku zinahamia nchi jirani ya Kenya.

"Endapo Bandari ya Bagamoyo itajengwa, itapunguza foleni iliyopo sasa na gharama kwa wananchi wanaoagiza mizigo kutoka nje ambao wanalazimika kusubiri kwa siku mbili na zaidi mizigo yao kushushwa kutokana na msongamano," alisema.

Alimpongeza Rais Samia kwa malengo yake ya kuruhusu mazungumzo ya mradi huo kufanyika ili bandari hiyo ijengwe.

Diwani wa Kata ya Zinga unapotarajia kujengwa mradi huo, Mohamed Mwinyigogo, alieleza kuwa ujenzi huo ni moja ya chanzo cha mapato katika Halmashauri ya Bagamoyo, na kwamba uchumi utakua.

Mwinyogogo pia alisema wananchi wa mji wa Bagamoyo watanufaika hususani wenye hoteli na nyumba ambazo watapangisha na itawasaidia kukuza kipato na kuondokana na umaskini.

"Mimi naomba dua kwa Mwezi Mungu ajaalie kusiwe na mabadiliko kuhusu huu mradi, kwani kwa wanaBagamoyo utakuwa mkombozi wetu kiuchumi."

Naye Diwani wa Kiromo, Salumu Mikugo, alieleza kuwa pamoja na faida ya ajira kwa vijana kutakuwa na ongezeko la ujenzi wa viwanda katika Wilaya ya Bagamoyo.

"Halmashauri itapata mapato, uchumi utakua wafanyabiashara watakuza biashara zao kupitia mradi huu na uwekezaji utakaokuwapo kwenye viwanda, hii ni faraja kwetu wanaBagamoyo," alisisitiza. Alisema vijana wengi wamejikita kwenye bodaboda kutokana na kukosa ajira, hivyo uwapo wa bandari hiyo kutawafanya kuwa na ajira rasmi.

Mmoja wa wakazi wa Bagamoyo, Mzee Marijani maarufu 'Minjoli', alisema ujenzi wa bandari hiyo utaleta faida sio kwa Tanzania peke bali hata nchi za Afrika Mashariki, na kwamba uchumi utainuka kuanzia kwa wajasiriamali wadogo kwani watapata sehemu ya kuuzia vitu vyao.

Marijani ambaye ni mkazi wa Nianjema, anamwomba Rais pia kusaidia wakazi wa Mlingotini, Zinga na maeneo mengine ya mradi ambao hawajalipwa fidia hadi sasa kupisha mradi na waliolipwa kidogo waongezewe ili waendelee na maisha mengine.

Naye Mwinyihashimu Akida, mkazi wa Dunda, alisema wakazi wa mji wa Bagamoyo wamefurahia kauli ya Rais kuhusiana na mradi huo, ambao utakuwa mkombozi wao kiuchumi.

Ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo ulianzishwa na Rais wa awamu ya nne, Jakaya Kikwete, lakini awamu ya tano ya Hayati John Magufuli iliusitisha kwa maelezo kuwa haukuwa na maslahi kutokana na mikataba yake.



Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, akipita karibu na biashara ya mmoja wa wajasiriamali aliyepanga bidhaa zake karibu na mradi wa barabara ya mwendo kasi Mbagala Rangi Tatu jijini jana. PICHA: MAULID MMBAGA

# PAC yataka kamati ufuatiliaji

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

MWENYEKITI wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), Naghenjwa Kaboyoka, amelishauri Bunge kuunda Kamati ya Ufuatiliaji ili kuibana serikali kushughulikia hoja muhimu zinazoibuliwa na chombo hicho cha kutunga sheria.

Kaboyoka ambaye amekuwa kiongozi wa kamati hiyo tangu Bunge la 11, alitoa pendekezo hilo jana jijini hapa wakati wa uzinduzi wa Ripoti za Uwajibikaji kwa Mwaka 2019/20 zilizoandaliwa na Taasisi ya WAJIBU.

Alisema ni muhimu kuundwa kwa kamati hiyo kwa kuwa imeshuhudiwa kwa miaka mingi Bunge likiibua hoja muhimu dhidi ya serikali, lakini hazifanyiwi kazi huku kukionekana kukosekana mfuatiliaji wa utekelezaji huo.

"Mfano, angalia bajeti ya kilimo iliyopita (2020/21), imetolewa kwa asilimia mbili. Kilimo ni sekta ya uzalishaji ambayo inaajiri asilimia 65 ya Watanzania. Tupeleke fedha kwenye sekta zinazozalisha ili tuepuke maendeleo ya vitu badala ya maendeleo ya watu.

"Ninachoona sasa kinahitajika bungeni, tuwe na kamati inayofuatilia utekelezaji wa mapendekezo ya kamati zingine za Bunge.

"Kwa sasa PAC tunachambua Ripoti ya CAG, tunawasilisha mapendekezo yetu ambayo yanakuwa maazimio ya Bunge. Yasipotekelezwa itakuwaje?

"Tunachotaka tuwe na kamati ambayo itafuatilia 'haya maazimio ya Bunge yametekelezwa kiasi gani?' Na wale ambao wameshindwa kutekeleza wachukuliwe hatua.

"Na ninavyojua Rais wa sasa (Samia Suluhu Hassan) atalifanyia kazi hili kwa kushirikiana na Bunge. Na ningemwomba aelekeze fedha kwenye sekta zinazozalisha kikiwamo kilimo. Na tulime kibiashara," alisema.

Miaka mitatu iliyopita, Spika wa Bunge, Job Ndugai, aliunda kamati mbili za kufuatilia mwenendo wa uchimbaji na biashara ya gesi asilia na hali ya uvuvi wa Bahari Kuu nchini.

Miongoni mwa mapendekezo ya kamati hizo zilizobaini dosari nyingi zinazolitia taifa hasara ya mabilioni, ni kuchukuliwa hatua kwa mawaziri waliotajwa. Mapendekezo hayo hayajafanyiwa kazi.

# Kampuni ya ulinzi yaonywa wizi benki

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JESHI la Magereza limewaagiza askari wa Kampuni ya Ulinzi ya ShimaGuard, waliohitimu mafunzo ya uaskari kuacha kushawishiwa kuiba katika benki ikiwamo kuwaibia wateja, badala yake wakafanye kazi walioagizwa.

Aidha, jeshi hilo, limewataka askari hao watakaopangiwa kwenda kulinda katika ATM za Benki mbalimbali nchini, kuacha tabia ya kuwaomba fedha wateja wanaokwenda kutoa fedha katika ATM hizo.

Hayo yalisemwa na Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Magereza na Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Magereza (SHIMA), Chacha Jackson, wakati akifunga mafunzo ya askari wahitimu 104 kutoka Kampuni ya ShimaGuard waliohitimu mafunzo ya uaskari.

Kamishna msaidizi Chacha alisema nidhamu katika jeshi ni jambo la msingi sana katika kazi na ndio itawajengea uwezo wa kuaminiwa na watu pale watakapokwenda kufanya kazi.

Alisema kumekuwapo na tabia ya baadhi ya askari wa kampuni ya ulinzi kuingia tamaa na kurubuniwa kufanya vitendo vya wizi dhidi ya wateja wanaokwenda kuchukua fedha benki au kwenye ATM.

Msikubali kufanya hivyo badala yake fuateni sheria mlizofundishwa katika kazi.

Akizungumzia kuhusu askari wa ulinzi kuomba hela kwa wateja kwenye ATM, alisema asingependa kusikia tabia hiyo na kama ipo inapaswa kuachwa.

Naye Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Shima Guard, Msepwa Omary, alisema mafunzo hayo yalianza Juni Mosi ambapo jumla ya wahitimu 104 wamemaliza huku wahitimu wengine nao wamehitimu katika mikoa ya Mwanza na Dar es Salaam.

Aliwataka kwenda kufanya kazi badala ya kujiingiza katika vitendo viovu, ambavyo vitaliletea sifa mbaya shirika na Jeshi la Magereza.

# HABARI KITAIFA

## Mpango kumwakilisha Samia kongamano kizazi cha usawa

**Na Salome Kitomari**

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, anatarajia kumwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan, katika kongamano la kihistoria la kizazi cha usawa, litakalofanyika kesho jijini Paris, Ufaransa.

Aidha, katika mkutano huo wa siku tatu, Makamu wa Rais atawasilisha mambo sita ambayo ndiyo msimamo wa nchi katika haki za binadamu na kiuchumi.

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula, aliyasema hayo jana Dar es Salaam, wakati wa mkutano wa waandishi wa habari uliojumuisha Balozi wa Ufaransa nchini, Frederic Clavier na Mwakilishi Mkaazi wa UN Women nchini, Hodan Addou.

Alisema kongamano hilo litakuwa mahsusi kuangazia masuala ya jinsia katika kizazi cha sasa na kijacho, na kwamba wakuu wa nchi, asasi za kiraia na Mashirika ya Umoja wa Mataifa (UN), watafanya tathmini ya miaka 25 ya Azimio la Beijing, China mwaka 1995.

"Safari hii imeamuliwa kwamba kuliko kwenda kwenye mkutano na kutoa hotuba, wakuu wa nchi, wakuu wa mashirika na vyombo vya habari wataweka utayari wao. Tanzania Rais Samia amedhamiria kuweka nguvu kubwa kwenye eneo la nguvu ya wanawake katika uchumi na haki za binadamu," alisema.

Balozi Mulamula alisema haki hiyo ni usawa wa kushiriki kwenye uchumi, unaozingatia haki, maendeleo ya nchi, kujenga ubia na Jumuiya za Kimataifa ili kufanikisha malengo nchi iliyojiwekea.

Naye Balozi wa Ufaransa, Clavier alisema kongamano la kizazi cha usawa, ni kongamano la kihistoria, linakuja miaka 26 baada ya Azimio la Beijing kushindwa kupunguza pengo la usawa wa jinsia katika nchi mbalimbali, duniani kote.

"Kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa, linalojihusisha na masuala ya wanawake (UN Women), Mexico na Ufaransa ndizo nchi zilizobuni na kuanzisha kongamano," alisema.

"Kongamano hili la aina yake lenye lengo la kufikia usawa wa kijinsia ifikapo mwaka 2030 litakuwa fursa ya kuwaunganisha kwa pamoja, wadau mbalimbali kwenye meza moja, kupata suluhu ya pamoja kutoka serikali, sekta binafsi, mashirika ya vijana, mashirika ya asasi za kiraia na wanaharakati watetezi wa wanawake," alisema.

Aidha, Balozi Clavier alisema yako mafanikio mengi katika miaka 26, lakini mafanikio hayo bado hayatoshi na ndiyo maana tunahitaji hatua za pamoja na kutokuwaacha wadau wengine nyuma.

"Vijana ndiyo walengwa, wahamasishaji ndiyo wanao paza sauti na kusikika, wanaowainua wale ambao wamenyamazishwa, wamenyanyapaliwa kwa muda mrefu na kwa hali hiyo, vijana husukuma mabadiliko," alisema.

"Kizazi hiki kipya kinachukua fursa kujenga maisha yao, jamii na kujenga uchumi na mifumo ya kuimarisha haki za binadamu na kuhakikisha hakuna mtu anayeachwa nyuma. Mashirika yanayoongozwa na vijana, yanayo jukumu la kuchochea na kuhakikisha uendelevu wa harakati za kuhakikisha usawa wa kijinsia unapatikana," alisema.

## Bunge lakataa tozo ya 20,000/- jando, unyago

**Na Godfrey Mushi, DODOMA**

MALIPO ya ada ya shughuli za jando na unyago ya Sh. 20,000 wanayotozwa wananchi na baadhi ya halmashauri za wilaya kama chanzo cha mapato, yamelichefua Bunge.

Kutokana na ugharimiaji wa shughuli hizo mara nyingi kufanywa na jamii kwa kujibana ili kufanikisha azma ya mafunzo kwa kijamii, Bunge limekataa wananchi kuendelea kutozwa ada hiyo.

Katazo hilo lilitangazwa jana na Bunge, kupitia azimio lililowasilishwa na Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo, Ridhiwan Kikwete.

"Shughuli hizo, si shughuli za kijamii na lengo lake ni kutoa mafunzo ya maisha ya kijamii kwa vijana. Ugharimiaji wa shughuli hizo mara nyingi ni kwa wanajamii kujibana kwa mambo mbalimbali ili kufanikisha azma ya mafunzo ya kijamii.

"Kwa sababu hiyo, kutoza ushuru au malipo yoyote kwa shughuli za aina hiyo zinazotokana na wananchi kujibana, ni jambo lisilo na maana yoyote kwa utekelezaji wa sheria na uendeshaji wa shughuli za umma kwa jamii." Katika uchambuzi wa kamati hiyo, Ridhiwan ambaye ni Mbunge wa Chalinze (CCM), alisema uchambuzi wao umebaini kuna jumla ya sheria ndogo kumi na moja (11) zina hoja inayohusu dosari ya kuwa na vifungu visivyozingatia uhalisia.

Alisema mfano wa sheria ndogo zenye hoja hiyo ni Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru za Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto ya Mwaka 2020, iliyotangazwa katika Gazeti la Serikali (GN. Na 1024/11 Desemba, 2020) zilizotungwa chini ya (Sheria ya Fedha ya Serikali ya Mitaa), (Sura 290).

Akisisitiza kutokubali kuendelea kutumika kwa sheria hiyo, Ridhiwan alieleza: "Katu, Bunge ambalo ni chombo cha uwakilishi wa wananchi, haliwezi kuachia mamlaka zilizoruhusiwa na Sheria ya Bunge zitunge sheria ndogo zisizoakisi shabaha na madhumuni ya sheria mama.

"Tozo za ada ya shilingi 20,000 kwa tukio la jando na unyago, si jambo lenye maana na mantiki yoyote katika maisha ya jamii zilizopo za wakazi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto.

"Kuendelea kutumia sheria ndogo hizo na kuwatoza wananchi ada ya shughuli za jando na unyago ni kuongeza kero na adha kubwa kwa wananchi.

Spika wa Bunge, Job Ndugai, alikazia suala hilo kwa kueleza kuwa suala hilo limegeuzwa kuwa chanzo cha mapato kwa halmashauri jambo ambalo si zuri.

Mbunge wa Mahonda, Ramadhani Suleiman Ramadhani, alisema shughuli za jando na unyago zimefanywa au zimegeuzwa kuwa chanzo cha mapato wakati elimu hiyo inawapa darasa wahusika la namna ya kwenda kuishi. Mbunge wa Kiteto (CCM), Edward Ole Lekaita, alisema licha ya kuwa sheria hiyo ilipitishwa Desemba mwaka jana ipo haja ya kuangaliwa baadhi ya maeneo ili ifanyiwe marekebisho.

Mbunge wa Viti Maalum (CCM) Najma Giga, alishauri sheria hiyo kuangaliwa upya ili kuondoa tozo hiyo ambayo inaonekana kuwa kandamizi kwa wahusika au jamii kwa ujumla.

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

**MAOMBI YA TAARIFA YA KUONYESHA NIA YA KUTOA HUDUMA YA KUANDAA MPANGO KAZI WA ZIADA WA UHAMISHAJI WA WATU NA MAKAZI PAMOJA NA MPANGO WA UREJESHAJI WA UWEZO WA KUJIKIMU KWA AJILI YA MRADI WA BOMBA LA MAFUTA GHAFI LA AFRIKA MASHARIKI (EACOP) KUMBUKUMBU NA: 0010006870**

TOTAL East Africa Midstream B.V (Kampuni) Tanzania, kampuni ya kimataifa ya nishati, inaalika makampuni/taasisi yenye utaalamu na uzoefu katika Uhamishaji wa Watu na Makazi Pamoja na Urejeshaji wa Uwezo wa Kujikimu kutuma nia ya kutoa huduma katika Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

Mradi wa EACOP unajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba litakalofukiwa chini linalokatisha mipaka ya nchi mbili na litakalo safirisha Mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka pwani ya Mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kusafirisha Mafuta hayo katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoa wa Tanga nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni karibia kilomita 1,443, kati hizo kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania. Ardhi imeshatwaliwa katika rasi ya Chongoleani kwa ajili ya ujezi wa kitua cha kuhifadhia mafuta kilicho pembezoni mwa bahari na kugusa jamii ambazo zinategemea ardhi pamoja na bahari ili kuweza kujikimu.

**MAELEZO MAFUPI YA MAWANDA YA HUDUMA:**

Kampuni inahitaji huduma kutoka kwa makampuni/taasisi yaliyobobea/iliyobobea katika Uhamishaji wa Watu na Makazi Pamoja na Urejeshaji wa uwezo wa kujikimu kwa lengo la:

- Kuandaa Mpango Kazi wa Uhamishaji wa Watu na Makazi (RAP) wa ziada kwa ajili ya Waguswa wa Mradi waliopo katika jamii inayoishi kwenye Rasi ya Chongoleani.
- Kufanya tathmini ya uwezo wa kujikimu (katika matumizi ya ardhi Pamoja na bahari) katika jamii.
- Kuandaa Mpango wa Urejeshaji wa Uwezo wa Kujikimu (LRP) kwa ajili ya Jamii ya Rasi ya Chongoleani iliyoguswa na Mradi.

**VIGEZO MUHIMU:**

Makampuni yanayoonyesha nia yanaalikwa kutuma maombi pamoja na nyaraka zifuatazo:

- Uthibitisho wa kuandaa Mipango Kazi ya Uhamishaji wa Watu na Makazi Pamoja na Mipango ya Urejeshaji wa Uwezo wa Kujikimu katika miradi ya viwanda barani Afrika.
- Uthibitisho wa uzoefu wa kusanifu mipango ya uhamishaji wa watu na makazi pamoja na mipango ya urejeshaji uwezo wa kujikimu katika miradi mikubwa ya ujenzi inayodhaminiwa.
- Afisa anayependekezwa pamoja na wataalam wa maswala ya ardhi na uwezo wa kujikimu katika matumizi ya ardhi na bahari pamoja na uzoefu wao katika kutoa huduma kwenye eneo husika.
- Uthibitisho wa usajili wa watekelezaji wa ngazi za juu katika taasisi za kitaaluma za Kitanzania au shirikisho.
- Usajili katika Kanzi Data ya Watoa Huduma wa Ndani ya EWURA (LSSP) katika kipindi cha kuwasilisha majibu ya nia kwa ombi hili yanahimizwa.

Makampuni zenye nia, uwezo na rasilimali za kutoa huduma zilizotajwa hapo juu zinatakiwa kutuma taarifa ya kuonyesha nia iliyoandaliwa kwa lugha ya kiingereza pamoja na nyaraka tajwa kupitia barua pepe: **talal.mufti@external.totalenergies.com** (ukubwa usiozidi MB20) hadi kufikia saa **11:00 jioni** Majira ya Afrika Mashariki, tarehe **13 Julai 2021.**

**Muhimu: Kwa ajili ya kutengeneza orodha ya makampuni ya Awali yenye vigezo, Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yenye nia. Mwaliko kwa Makampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa Makampuni ya Awali yenye vigezo baada ya makampuni hayo kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA).**

216333502

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kongole Samia, tujengee mifumo na taasisi imara

Rais Samia Suluhu Hassan, ametimiza siku 100 madarakani akiwa ni rais wa kwanza mwanamke Afrika Mashariki na Kati.

Ndani ya siku 100 ameonyesha uwezo mkubwa wa utendaji kazi katika kuleta umoja wa kitaifa kwa vitendo, ikiwamo kuweka wazi juu ya uwapo na utayari wa serikali kushughulikia ugonjwa wa corona, kwa kuunda kamati ya kitaalamu kuishauri serikali ambayo ilishatoa ushauri wake.

Pia, ameshalieleza taifa kuwa corona ipo na kila mmoja anapaswa kuchukua tahadhari kwa kuvaa barakoa, kuepuka misongamano, kunawa mikono kwa sabuni na maji tiririka na kutumia vipangusa mikono.

Rais amekutana na makundi mbalimbali kama wazee, wanawake, vijana, Baraza la Maaskofu Tanzania (TEC) na Jumuiya ya Wafanyabiashara na Wahariri wa Habari Tanzania na kote huko walitoka na kicheko kwa kuwa kero za msingi zimeshughulikiwa na zinaendelea kushughulikiwa.

Lakini amefanikiwa kuimarisha diplomasia ya nje ikiwamo kwenda kuhutubia Bunge la Kenya na kueleza umuhimu wa kuendelea kushirikiana na jinsi nchi hizo zinavyotegemeana katika mambo mengi, pia amehudhuria vikao vya kimtandao na moja kwa moja na wakuu wa taasisi za kimataifa, mabalozi na marais. Yote hiyo ni katika kuendelea kuonyesha nafasi ya Tanzania katika muktadha tofauti tofauti.

Eneo lingine ni usawa wa kijinsia, ambao aliahidi kuongeza idadi ya wanawake kwenye nafasi za maamuzi, na hilo limedhihirika kwenye uteuzi wa Mawaziri, Makatibu Wakuu, Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakuu Wakuu wa Wilaya, na hasa kuzingatia mambo ya msingi ya Muungano hasa kwa wizara ambazo zinahitaji uteuzi wa pande zote, na tunaamini idadi itazidi kuendelea kwa nafasi zilizosalia.

Eneo lingine ni la kodi, ambalo aliweka wazi kuwa hatakubali kodi ya dhuluma na baada ya muda Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ilitangaza kufungua akaunti za wafanyabiashara zilizokuwa zimeshikiliwa.

La muhimu ni kwenye utawala wa sheria, ambao tumeona jitihada za kumaliza na kufutwa kesi ambazo zimekaa muda mrefu bila kukamilia, huku muhimili wa Mahakama unatenda kazi zake kwa ufanisi na sasa haki inatamalaki.

Mifano michache ni uamuzi wa Mahakama ya Rufani kuamuru serikali kurejesha fedha walizotozwa faini viongozi wa chama kimoja cha siasa, na jana kada wa chama hicho, aliachiwa huru na Mahakama Kuu Kanda ya Mbeya na kuachiwa kwa Mashekhe wa Uamsho 36.

Tunauthubutu wa kusema tunamshukuru Mungu kwa ajili yake, na tunampa hongera kwa kuliongoza taifa kwa umahiri mkubwa, ambao umeleta tumaini na faraja baada ya msiba mzito wa Rais wa awamu ya tano, Hayati Dk. John Magufuli, kuondoa hofu ya kuongozwa na mwanamke na kuendelea kujenga ujasiri kuwa wanawake wanaweza, kubwa ni kuwaamini na kuwapa nafasi.

Pamoja na mafanikio hayo, sasa tunapenda kuona ikijengwa mifumo na taasisi imara, ili mazuri yanayoonekana na kufurahiwa na Watanzania yabaki kwenye mifumo hata akija kiongozi mwingine hawezi kubadili na nchi itakuwa na mwendelezo.

Nchi zilizoendelea zimewekeza kwenye taasisi na mifumo imara na siyo mtu imara, kiasi kwamba hata alivyoondoka kiongozi, hakuna kinachoharibika.


Pia, kilio cha Katiba Mpya kimekuwa cha muda mrefu na mwaka 2014 Bunge Maalum la Katiba ambalo Rais Samia alikuwa Makamu Mwenyekiti, lilikamilisha Katiba Pendekezwa, lakini wapinzani walisusia mchakato na kutoka nje ya Bunge na kutaka rasimu ya wananchi iheshimiwe.

Pamoja na mazuri mengi, ni muhimu kilio hiki kikategewa sikio kwa kuwa mchakato ulishaanza na ulitafuna mabilioni ya Watanzania, lakini Katiba iliyopo sasa ni ya miaka 44, kuna mambo yanahitaji marekebisho kwa kuzingatia mabadiliko mengi na ongezeko la watu.

Kongole rais na endelea kudumisha furaha ya Watanzania kwa kutatua kero za msingi, ili watu wafurahie na kujivunia kuzaliwa na kuishi nyumbani na moja kwa moja watakuwa wazalendo na kukipenda cha chao kwa kuwa wananufaika.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Fursa wajawazito kurejea shuleni iwe ni funzo pia

Na Sabato Kasika

SERIKALI imekuja na utaratibu mpya utakaowawezesha wanafunzi waliokatiza masomo kutokana na sababu mbalimbali, ikiwamo ujauzito, warejee masomoni.

Utaratibu huo ni wa kupitia vyuo vya maendeleo ya jamii, hivyo kutokana na uamuzi huo, wakuu wa vyuo hivyo wahakikishe kuwa wanafunzi wa kike walioshindwa kuendelea na masomo yao kwa sababu wanachukuliwa na kuendelea na masomo.

Ili kufanikisha lengo hilo, wakuu wa vyuo hivyo wanaelekezwa na serikali kutekeleza maelekezo hayo kwa kudahili wanafunzi hao kupitia mpango wa elimu haina mwisho ifikapo mwaka 2022.

Vyuo hivyo pia vinatakiwa kuwa vimesajiliwa kama vituo vya kufanyia mitihani ya kidato cha pili na cha nne, ili kuwawezesha wahusika wote kufanya mitihani na hatimaye kusonga mbele katika elimu.

Hatua zilizochukuliwa na serikali kwa ajili ya wanafunzi hao ni za kupongeza, kutokana na ukweli kwamba, elimu ndiyo msingi wa maisha ya mtoto na pia urithi na maisha bora kwa mtoto ni elimu na si fedha, magari wala nyumba.

Kwa maana hiyo, kila mzazi na mlezi ni muhimu waifanye elimu kuwa kipaumbele kwa watoto wao, kwani ndiyo itakayoonyesha mwelekeo wa baadaye wa maisha ya watoto hao.

Taratibu za shule haziruhusu mwanafunzi kubeba mimba, lakini taarifa kutokana na maeneo mbalimbali nchini, zimekuwa zikionyesha jinsi ambavyo baadhi ya wanafunzi wamekuwa wakikumbwa na tatizo hilo.

Kumekuwapo na mjadala kutoka wadau wa elimu, wakiwamo wanaotaka serikali iruhusu wanafunzi wanaopata ujauzito wakiwa shuleni waendelee na masomo baada ya kujifungua, huku wengine wakipinga.

Sasa kwa kuwa serikali imeamua kuja na utaratibu mpya wa kuwawezesha waliokatiza masomo kwa sababu mbalimbali ikiwamo ya mimba kuendelea na masomo, ni vyema wazazi, walezi na wanafunzi wasipoteze fursa hiyo.

Vilevile wanafunzi ambao hawajakumbwa na tatizo hilo, isiwe fursa mbaya kwao kujiachia au kujihusisha na ngono katika umri mdogo wakijua kwamba, wana nafasi ya kujiunga na vyuo vya maendeleo ya jamii kuendelea na masomo baada ya kujifungua.

Ni kweli kutowaruhusu kusoma wanafunzi waliopata mimba shuleni, ni kuwanyima haki ya kupata elimu, lakini zinapopatikana nafasi kama hiyo iliyotolewa na serikali, ni muhimu kuitumia kikamilifu.

Hivyo ni muhimu kila mwanafunzi kuchukua tahadhari zaidi ili kuepuka tatizo hilo, kwa kuwa hali hiyo inamfanya asitimize ndoto yake katika elimu na pia wazazi na walezi wawe mstari wa mbele kuhimiza maadili mema.

Imekuwa ikidaiwa kuwa baadhi ya kesi za wanafunzi kupewa mimba huwa zinahusisha wao wenyewe, lakini nyingine hugusa wazazi na walezi ambao huwatumia kama kitega uchumi chao.

Wakati serikali imekuja na njia nyingine ya kuwasaidia wale waliopata ujauzito na kukatisha masomo, ni vyema nafasi hiyo ikatumiwa vizuri ili kila mwanafunzi aweze kutimiza ndoto yake katika elimu.

Ni vyema wazazi na walezi watoe elimu ya afya ya uzazi kwa watoto wao, ili iwasaidie kuwa makini, kwa kuwa inawezekana wengi wao hawana elimu hiyo, matokeo yake wanashiriki ngono wakiwa na umri mdogo.

Katika maisha ya sasa hakuna usiri bali ni uwazi na ukweli, ili kusaidia watoto wa kike kuepuka kujiingiza kwenye ngono na kusababisha wakatize masomo na hivyo kujikuta wakikwama kutimiza ndoto zao.

# Makalla: Masoko yaruhusu magari

**Na Maulid Mmbaga**



MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, amewataka wasimamizi wa masoko yaliyokamilika waruhusu magari yanayouza bidhaa za jumla kuingia katika sehemu hizo.

Lengo ni kuchagiza biashara kutokana na wafanyabiashara kulalamika kuwa maeneo hayo hayana mzunguko wa kibiashara.

Aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, alipofanya ziara ya kikazi katika Manispaa ya Temeke, ambapo alikagua masoko matatu yakiwamo soko la Kijichi, Mbagala Kuu na Makangalawe yaliyogharimu zaidi ya Sh. bilioni 6 katika utekelezaji wake na kwamba, serikali imetumia fedha nyingi kutengeneza masoko hayo, hivyo hayawezi kukaa bila kutumika.

Alisema nia ya serikali katika kuweka miundombinu ya masoko ni kuhakikisha kuwa wananchi wanakuwa na mazingira rafiki ya kuwawezesha kufanya biashara zao, hivyo amemwagiza Mkuu wa Wilaya hiyo, Joketi Mwegelo, kuwaagiza Wakala wa Usafirishaji wa Ardhini (LATRA) kuratibu zoezi la kufanikisha daladala kufika katika maeneo ya masoko ili kuongeza mzunguko wa watu.

"Katika sehemu kama hizi za masoko bila kuwa na mzunguko mkubwa wa watu biashara haziwezi kufanyika hivyo, LATRA hakikisheni ndani ya wiki mbili daladala zifike kuleta watu katika masoko haya, pia ofisa masoko hakikisha unafuatilia changamoto zinazokwamisha biashara katika masoko na uzitatue.

"Haiwezekani ofisa masoko yupo anapokea mshahara, lakini masoko hayafanyi kazi kama inavyotarajiwa...mimi naamini katika matokeo baada ya wiki mbili nitarudi tena hapa nikute changamoto zote zinazokwamisha biashara katika maeneo haya zimetatuliwa, daladala zifike, magari ya bidhaa za jumla na rejareja zifike biashara ifanyike," alisema Makalla.

Aliongeza kuwa kwa wale wafanyabiashara walioweka biashara zao katika eneo la ujenzi wa barabara ya mwendokasi Mbagala waziondoe maramoja ili kuwaondolea kero makandarasi watimize majukumu yao ipasavyo.

# Waliokatisha masomo waomba unafuu ada VETA

**Na Elizabeth Zaya**

BAADHI ya wanafunzi waliokatisha masomo kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo ujauzito, wameiomba serikali kuondoa au kupunguza ada katika Vyuo vya Ufundi (VETA), ili kuwapa fursa ya kwenda kujipatia ujuzi, baada ya kukosa fursa ya elimu katika mfumo rasmi.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti na Nipashe katika kata za Kerege na Mapinga wilayani Bagamoyo Mkoa wa Pwani, walisema wanakatisha masomo yao kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo umaskini, hivyo ni vema serikali ikawapa nafasi ya pili ya kupata elimu ya ufundi kwa gharama nafuu.

Aisha Hassan wa Kijiji cha Udindivu, alisema alikatisha masomo akiwa kidato cha kwanza mwaka 2019 kutokana na kuelemewa na jukumu la kulea wadogo zake, baada ya mama yake kuachana na baba yake, hivyo kuondoka nyumbani.

"Sikupenda kuacha shule, isipokuwa nilizidiwa na majukumu. Kwetu tupo watoto wanne na mimi ndiye wa kwanza kuzaliwa, wazazi wangu waliachana tangu nikiwa mwezi wa sita kidato cha kwanza... mama aliondoka na kutuacha na baba na baada ya hapo mimi ndiye nikabaki nawahudumia wadogo zangu," alisema Aisha.

"Niliendelea kwenda shuleni, lakini ilipofika mwezi wa 10 mwaka huo 2019 niliacha kwenda kwa sababu nilishindwa kujigawa, kati ya majukumu ya nyumbani na ya shule na nikawa nafeli sana." Aisha alisema kwa sasa anatamani kwenda kusomea ufundi, lakini kinachomkwamisha ni kukosa ada ya kulipia mafunzo ya ujuzi anaoutamani.

"Natamani kusomea ufundi wa umeme, lakini sina ada ya kulipia, ninaomba serikali ifikirie namna ya kupunguza ada kwenye vyuo vya ufundi au kuiondoa kabisa ili kila mtu anayeshindwa kupata fursa ya elimu kwenye mfumo rasmi angalau asikose na ujuzi hasa sisi tunaotoka katika familia duni," alisema Aisha.

Zainabu Juma, alisema yeye ni mjane na ana watoto wanne, na mmoja tu ndiye aliyefanikiwa kuhitimu kidato cha nne, mmoja aliishia darasa la saba na wengine wawili waliishia kidato cha pili.

Kwamba alitamani kuwapeleka vyuo vya ufundi ili wapate ujuzi wa kuwasaidia kupata kazi ya kuendesha maisha yao, lakini ameshindwa kutokana na kuwa na kipato kidogo.

"Watoto wanatamani kwenda kujifunza ufundi, lakini tulipokwenda kuuliza kwenye vyuo vya ufundi, tuliambia ada ambayo siwezi kumudu, kwa hiyo bado niko nao nyumbani wananisaidia tu kazi ndogo ndogo za ujasiriamali kwa ajili ya kuendesha maisha yetu ya kila siku," alisema Zainabu.

"Tunashukuru serikali imeondoa ada kwenye hizi shule za msingi na sekondari, ninaomba ingeangalia pia na huku kwenye vyuo vya ufundi ipunguze ada ili watoto hasa wa familia maskini wapate nao ujuzi."

# Afutiwa adhabu ya kuajiri raia wa kigeni bila kibali

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Masijala ya Mtwara imemfutia adhabu mmiliki wa Shule ya Southern Star, Reyness Oluoch, aliyetiwa hatiani kwa kosa la kumwajiri mumewe raia wa Burundi bila kibali.

Reyness amedai hakuwa anajua kwamba mumewe siyo raia, hakuwa na namna yoyote ya kujua hilo kwa kuwa hakuwa na alama maalum inayoweza kumtambulisha uraia wake.

Uamuzi huo wa mahakama ulitolewa hivi karibuni na Jaji Paul Ngwembe, baada ya kupitia hoja za mrufani na hoja za wajibu rufani na kubaini kwamba mahakama ilikosea kumtia hatiani na kupewa adhabu ya kwenda jela miezi mitano au kulipa faini Sh. 500,000.

Wakili Rainery Songea akimwakilisha mrufani katika hoja zake, alidai Jamhuri ilishindwa kuthibitisha kwamba aliajiri raia wa Burundi bila kuacha shaka.

Pia, alidai mahakama ilikosea kuhamishia jukumu la kuthibitisha kwamba Nimrod Elite hakuwa raia wa Tanzania kwa mshtakiwa ama mrufani.

Anadai mrufani hakuwa anajua kwamba mume wake ni raia wa Burundi na kwamba mumewe hakuwa na alama maalumu inayomtambulisha kwamba ni raia wa Burundi na hakuwa na namna nyingine ya kutambua hayo. Wakili Songea alitoa cheti cha ndoa kati ya mrufani na Nimrod na aliiomba mahakama ikubali rufani na imfutie adhabu.

Akiiwakilisha Jamhuri, Wakili Wilbroad Ndunguru, alidai mahakama haikukosea kumtia hatiani na kumpa adhabu mrufani, ushahidi unaonyesha kwamba mrufani aliajiri raia wa kigeni bila kibali na kwamba lilikuwa jukumu lake kujua uraia wa mume wake.

Jaji Ngwembe alipoanza kusoma hukumu alipitia eneo dogo la ushahidi ambao ulielezea kwamba mrufani ni mmiliki wa Shule ya Msingi ya Southern Star na Nimrod Elite ni Meneja wa shule hiyo.

Mrufani anadai katika maisha yao mumewe hakumweleza kuwa ni raia wa Burundi, alimwambia ni raia wa Tanzania na anatokea Kigoma Ujiji, wazazi wake walikuwa wakiishi Yombo Machimbo.

"Eneo hilo la ushahidi linaonyesha mrufani hakuwa akijua kwamba mumewe ni raia wa kigeni, Hakimu alitakiwa kujiridhisha kwamba mshtakiwa alikuwa anajua kosa alilofanya kabla ya kufikia uamuzi.

"Jamhuri walitakiwa kuthibitisha mshtakiwa alikuwa na nia ovu, mahakama ya chini ilikosea hivyo mahakama hii inamfutia mrufani adhabu aliyopewa na kuamuru faini ya Sh. 500,000 aliyolipa badala ya kwenda jela arejeshewe," alisema Jaji Ngwembe.


Tpb Bank
Grow with us

TPB BANK PLC

**TAARIFA KWA UMMA**

**Mabadiliko ya Tarehe ya Uzinduzi wa Benki Mpya ya Serikali**

**Benki ya TPB** inapenda kuutangazia umma kuwa uzinduzi wa benki mpya ya Biashara ya Serikali uliokuwa ufanyike **tarehe 30 Juni 2021** katika ukumbi wa Kimataifa wa Mwalimu Julius Nyerere sasa umesogezwa mbele hadi tarehe **14 Julai 2021.**

Tunaomba radhi kwa usumbufu wowote utakao jitokeza

**Imetolewa na**
**kitengo cha mawasiliano cha Benki**
**Simu: 0762-283836**

216334102

# Korti yaamuru NICOL kulipwa mil. 580/-

**Na Hellen Mwango**

KAMPUNI ya NICOL imeshinda kesi ya mkopo wa Sh. milioni 580 iliyokomboa kwa ajili ya kampuni ya Twiga Feeds Limited inayojihusisha na biashara ya kuku, iliyopata kutoka kwenye Mfuko wa Jamii (SATF).

Uamuzi huo ulitolewa na Mahakama Kuu Division ya Ardhi, baada ya mlalamikaji Kampuni ya NICOL, kupinga madai yaliyotolewa na kampuni ya Twiga Feeds Limited na Abcon Chemicals Limited, walalamikaji.

Awali, Jaji Elinaza Luvanda aliziamuru kampuni mbili zinazolalamika kulipa kiasi cha Sh. milioni 580 pamoja na riba yake kwa kampuni inayolalamikiwa, baada ya kutupilia mbali kesi ya madai na nafuu zilizokuwa zikitafutwa, akisema walalamikaji walishindwa kuithibitishia mahakama baada ya kutoa ushahidi wao.

"Kampuni inayolalamikiwa ina haki ya kulipwa Sh. milioni 580 pamoja na riba ya asilimia 18 kwa mwaka kuanzia mwaka 2009. Kesi ya msingi ilitupiliwa mbali na madai kinzani yameshinda," alisema Jaji Luvanda.

Katika kesi hiyo, walalamikaji walikuwa wakiiomba Mahakama Kuu kutamka kwamba kiasi cha Sh. milioni 580 zilizolipwa na mlalamikiwa kwa SATF zilikuwa mchango wa NICOL kwenye mradi wa pamoja wa uwekezaji, na kwamba haukuwa mkopo.

Waliiomba mahakama kutamka kwamba kushindwa kwa mradi wa pamoja wa uwekezaji kulisababishwa na mlalamikiwa mwenyewe, na kwamba riba na adhabu zinazosemwa zinatokana na fedha dhidi ya walalamikaji ni batili na hazikuwapo, na kwamba Sh. milioni 580 zilizolipwa na mlalamikiwa hazikutakiwa kurejeshwa.

Aidha, walalamikaji waliiomba mahakama itamke kwamba mali iliyokuwa imewekwa rehani kwenye kiwanja eneo la viwandani Mbezi, Dar es Salaam, ilikuwa imefanywa kwa udanganyifu na ilikuwa batili, na kwamba wanaiomba mahakama itamke kwamba iachiwe.

Kwa upande mwingine, mlalamikiwa kwenye maelezo ya utetezi wake wa kimaandishi, kupitia wakili wake, Benjamin Mwakagamba, kwenye madai kinzani anaiomba mahakama kutoa uamuzi na kuwaamru walalamikaji walipe kiasi cha Sh. 2,403,123,177, kikiwa ni kiasi ambacho kilikuwa hakijalipwa pamoja na riba ya mkopo.

Katika hukumu yake, Jaji Luvanda alikataa ombi la walalamikaji kwamba fedha hizo hazikuwa mkopo uliotolewa, bali zilikuwa zimetolewa na mlalamikiwa kwa ajili ya mradi wa pamoja kuhusiana na kuanzishwa kwa taasisi ya elimu ya juu, iliyoitwa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (U-TAN).

## NIT, vyuo vya Kenya kushirikiana

**Na Mwandishi Wetu**

CHUO cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) kimeingia katika makubaliano ya Ushirikiano (MoU) na vyuo viwili kutoka Kenya ili kukuza ushirikiano katika taaluma na shughuli za utafiti.

Akizungumza na waandishi wa habari katika kampasi kuu ya NIT jijini Dar es Salaam jana, Mkuu wa Chuo hicho, Mhandisi Prof. Zacharia Mganilwa, alisema makubaliano kati ya vyuo vya Kenya Aeronautical College (KAC) na Kenya Coast National Polytechnic (KCNP) ni moja ya matakwa ya mradi wa EASTRIP, ambapo malengo makubwa ni kuleta mapinduzi kwenye elimu ya ufundi katika ukanda wa Afrika Mashariki.

"Tumesaini makubaliano na vyuo hivi vya Kenya ambapo kwa hivi sasa tutaweza kuanza kubadilishana walimu na wanafunzi kupitia mradi huu wa EASTRIP. Ingawa Chuo cha Kenya Aeronautical College hakipo kwenye mradi wa EASTRIP lakini kitaweza kutusaidia sisi kufikia malengo yetu kwenye eneo la mafunzo ya anga," alisema.

Akizungumzia mikataba yote miwili, Prof. Mganilwa alisema: "Mikataba hiyo ya ushirikiano imeainisha mambo ya ushirikiano kama kubadilishana walimu na wanafunzi pamoja na kusaidiana kujenga uwezo wa wanataaluma wa vyuo viwili hivi kwenye maeneo ambayo chuo kimoja kina uwezo zaidi, kuandaa mitaala ya pamoja na kufanya utafiti wa pamoja."

Alisema: "Kenya Polytechnic National Coast ni chuo kinachofundisha masomo ya usafiri wa maji, hivyo kwa ushirikiano na chuo chetu, tutapata nafasi nzuri ya kujifunza kutoka kwao katika eneo hilo la usafiri wa maji."

Prof. Mganilwa aliendelea kusema kuwa wataalamu hao kutoka vyuo hivyo vya Kenya wataweza vile vile kuboresha mitaala ya kufundishia katika Chuo cha NIT na wataalamu kutoka NIT wataweza kutoa ujuzi wao na kusaidia vyuo hivi vya Kenya kuboresha mitaala yao.

Benki ya Dunia imetoa mkopo wa Sh. bilioni 175 kwa Serikali ya Tanzania kwa ajili ya kuleta mapinduzi katika vyuo vinne vinavyotoa elimu ya ufundi hapa nchini.



Mwenyekiti wa Tanzania Patriotic Organization (TPO), Hamad Jiliu (kushoto) na Mwenyekiti wa Taasisi hiyo Mkoa wa Dar es Salaam, Aminatha Nombo (katikati), wakikabidhi msaada wa maji na vitu mbalimbali vilivyotolewa na taasisi hiyo mwishoni mwa wiki Kisarawe mkoani Pwani, kulia ni mlezi wa kituo cha Orphanage House cha Kisarawe, Veronica Kilango. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Agizo la Gwajima laanza kutekelezwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

BAADA ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, kutoa siku 30, kwa Baraza la Taifa la mashirika yasiyo ya kiserikali (NaCoNGO), kufanya uchaguzi, agizo hilo limeanza kutekelezwa kwa ngazi ya taifa umepangwa kufanyika Julai 8, jijini Dodoma.

Kabla ya Julai 10, uchaguzi wa baraza hilo kuanzia ngazi ya wilaya, mkoa hadi taifa utakuwa umekamilika na viongozi wapya kukabidhiwa rasmi ofisi.

Mwenyekiti wa kamati ya uchaguzi wa NaCoNGO, Wakili Flaviana Charles, alibainisha hayo jana jijini hapa wakati akitoa tathmini ya mwenendo wa uchaguzi wa baraza hilo ngazi ya wilaya.

Alisema kuwa Juni 7, mwaka huu Waziri Dk. Gwajima, alifanya uteuzi wa kamati ya mpito kwa ajili ya kuratibu na kusimamia uchaguzi wa Baraza la Taifa la mashirika yasiyo ya kiserikali.

"Kamati hiyo inaundwa na wajumbe 10, kutoka katika mashirika yasiyo ya kiserikali ya kitaifa na kimataifa na ilipewa siku 30, kufanikisha zoezi hilo," alisema wakili Charles.

Alisema kuwa jukumu la kamati hiyo ni kuratibu na kusimamia uchaguzi wa baraza hilo.

Mwenyekiti huyo alisema kuwa baraza litakaloundwa litakuwa na wajumbe 30, kati yao 26, kutoka katika mikoa yote ya Tanzania Bara na wajumbe wanne watachaguliwa kutoka katika makundi maalumu.

Alisema kuwa makundi hayo ni pamoja na mashirika ya kimataifa, watu wenye ulemavu pamoja na watoto na vijana.

"Kwa msingi huo taarifa hii inalenga kutoa tathmini ya mwenendo wa uchaguzi wa Baraza la Taifa la mashirika yasiyo ya kiserikali husani ngazi ya wilaya uliofanyika Juni 26, mwaka huu," alisema.

Aidha, alisema kuwa kwa ujumla uchaguzi ulifanyika kwa amani na utulivu katika wilaya zaidi ya 130, za Tanzania Bara ambapo kumekuwapo na mwitikio mkubwa na hamasa ya hali ya juu kwa wagombea na wapigakura.

"Tathmini ya ujumla katika wilaya zaidi ya 130, zilionyesha zoezi hilo kati ya watia nia watano waliochukua fomu za kuomba uongozi wa baraza jumla ya watia nia wanne walirudisha fomu hizo kwa msingi huo zoezi la kuchukua na kurudisha fomu lilifanikiwa kwa takribani asilimia 80," alisema.

Pia, alisema upigaji na kuhesabu kura ulifanyika Juni 26, mwaka huu, katika wilaya zote ndani ya mikoa 25 ya Tanzania Bara, isipokuwa katika wilaya za Mkoa wa Kigoma.

"Na kwa upande wa Ruvuma ambao kulikuwa na changamoto kadhaa na watafanya uchaguzi wiki hii niwaombe watu wa Ruvuma wajitokeze kwa wingi," alisisitiza.

Kadhalika, alisema kuwa katika baadhi ya wilaya uchaguzi haukufanyika kutokana na kukosekana wagombea wenye sifa waliojitokeza kuwania uongozi wa baraza au wengine kupita bila kupingwa.

# Wazalishaji wadogo kujadili ushiriki wao katika masoko

**Na Gwamaka Alipipi**

WAZALISHAJI wadogo zaidi ya 300 kutoka sekta ya uvuvi, ufugaji, kilimo, ufugaji na uvunaji wanatarajia kukutana mjini Dodoma kwa siku mbili, kujadiliana juu ya kuboresha ushiriki wao katika masoko ya ndani na nje.

Mbali na hilo, mkutano huo utafanikisha mjadala na utambuzi wa masuala ya kisera yanayowakandamiza wazalishaji wadogo katika ngazi tofauti na kukubaliana namna ya kuyashughulikia.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam, Mkuu wa Operesheni kutoka Jukwaa la Wadau wa Kilimo lisilo la Kiserikali (ANSAF), Honest Mseri, alisema mkutano huo utaanza Julai mosi, utafunguliwa na Waziri wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda.

"Zaidi ya wazalishaji 300 kutoka Tanzania Bara na Zanzibar watahudhuria sambamba na viongozi wa serikali hususani katika vikao vya kufungua na kufunga. Sambamba na mada kuu mkutano huu unalenga kujadili, kupanua ushiriki wa wazalishaji wadogo katika masoko ya ndani na nje," alisema Mseri.

Alisema mada ya mkutano huo imegawanyika katika maeneo manne ambayo yatazungumzia mifugo, uvuvi, kilimo, ufugaji wa nyuki na utumiaji wa rasilimali.

Mseri alisema lengo ni kuwezesha majadiliano ya kina kwa kila eneo husika ili kufikia lengo kuu la mkutano kwa ufanisi zaidi na kupata mapendekezo ya kisera hususani kwa maeneo ya huduma na taasisi wezeshi, kuongeza thamani, miundombinu ya usafirishaji na masoko, pamoja na mazingira wezeshi.

Mseri alisema: "Mkutano huu pia utachagiza suala la utetezi wa haki za wanawake, vijana na watu walio katika mazingira magumu vijijini katika kupata rasilimali zenye tija."

# Wakazi Dar, Pwani kupata hatimiliki ya ardhi siku moja

**Na Munir Shemweta**

WIZARA ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi itatoa hatimiliki za ardhi ndani ya siku moja kwa wananchi waliokamilisha taratibu za kupatiwa hati kwenye zoezi la urasimishaji makazi holela katika mikoa ya Dar es Salaam na Pwani.

Hati hizo zitatolewa wakati wa Maonyesho ya 45 Kimataifa ya Biashara maarufu Sabasaba.

Hayo yamebainishwa na Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini Wizara ya Ardhi, Lusajo Mawakabuku wakati akielezea mipango na mikakati ya wizara yake katika ushiriki wa maonyesho ya Sabasaba yanayofanyika viwanja vya Mwalimu Julius Nyerere vilivyopo Barabara ya Kilwa, Dar es Salaam. Alisema, kwa mwaka huu kwenye maonyesho ya Sabasaba, wizara imejipanga vizuri kuhakikisha inatoa na kutangaza huduma zinazotolewa ili kukidhi kiu wa wananchi watakaotembelea Banda la Wizara ya Ardhi.

Kwa mujibu wa Mwakabuku, wananchi wa mikoa ya Dar es Salaam na Pwani watakaoweza kupata Hatimiliki za Ardhi papo hapo katika Banda la Wizara (One Stop Shop), ni wale ambao maeneo yao yamefanyiwa urasimishaji na viwanja kupimwa.

Mwakabuku alisema nyaraka zinazotakiwa kwa mmiliki wa kiwanja anayetaka kupatiwa hati ni michoro ya mipango miji, ramani ya upimaji, fomu ya majirani, kitambulisho cha uraia pamoja na barua ya maombi. Kupitia maonyesho hayo ya Sabasaba Mwakabuku alisema, wananchi pia wataweza kununua ramani zenye wilaya mpya za Tanzania sambamba na wale wenye migogoro ya ardhi kuwasiliana moja kwa moja na makamishna wa ardhi wasaidizi wa mikoa ili kupata ufumbuzi wa migogoro katika maeneo yao.

Pia wananchi watakootembelea Banda la Wizara ya Ardhi watapata maelezo kuhusiana na huduma za Mipango Miji, maendeleo ya makazi, uthamini, upimaji na ramani pamoja na huduma za ukadiriaji na ulipaji kodi ya pango la ardhi ambapo watapatiwa ankara za malipo kwa ajili ya kwenda kulipia benki.



Mkuu wa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), Mhandisi Prof. Zacharia Mganilwa (kulia), akibadilishana mikataba na Mkurugenzi wa Chuo cha Kenya Aviation, Samson Aketch, baada ya kusaini makubaliano ya ushirikiano katika taaluma na shughuli za utafiti. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Elimu ya uthibitishaji ubora bidhaa kutolewa Sabasaba

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS) limetaja elimu na huduma mbalimbali zitakazotolewa kwa wananchi na washiriki wa Maonyesho ya Biashara ya Kimataifa ya Sabasaba ambayo yalianza jana kwenye Viwanja vya Mwalimu Julius Nyerere, jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na waandishi wa habari, Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Masoko wa TBS, Gladness Kaseka, alisema kupitia maonyesho hayo maofisa wa shirika hilo watoe elimu na huduma kuhusu udhibiti na uthibitishaji ubora wa bidhaa, uthibitishaji ubora wa mifumo na usajili wa majengo na bidhaa za chakula na vipodozi.

Kwa mujibu wa Kaseka huduma nyingine ni ya usajili wa papo kwa hapo wa majengo na baadaye utafuata ukaguzi wa majengo ya bidhaa za chakula na vipodozi na watapata kipata kibali ndani ya siku moja.

"Wananchi watakaofika kwenye banda letu watapata elimu kuhusu sayansi ya vipimo na elimu kuhusiana na huduma mbalimbali za maabara, taratibu na gharama za upimaji sampuli," alisema Kaseka.

Alitaja huduma zingine zitakazotolewa kwenye banda hilo ni za kutoa elimu juu ya ununuaji viwango na taarifa muhimu kwa bidhaa zinazouzwa nje ya nchi ili kuepukana na vikwazo vya kibiashara.

"Wale wanaohitaji huduma ya viwango wasisite kutembelea banda letu kutakuwa na huduma ya kuuza viwango na namna ya kushiriki kutoa maoni yao kama wadau kwa sababu jukumu hilo ni la kuandaa viwango ni sisi watumiaji pamoja na wataalamu wenyewe," alisema Kaseka .

Kwa mujibu wa Kaseka kupitia maonyesho hayo wananchi watajua ni njia gani ya kutumia kuweza kutoa maoni kuhusiana na viwango.

Kwa upande wa huduma za upimaji, Kaseka alisema kupitia fursa hiyo ya maonyesho wananchi watajua gharama za upimaji sampuli

# TRC kufanya tathmini gharama njia zilizofungwa

BUNGE limeelezwa kuwa katika mwaka wa fedha 2022/23, Shirika la Reli Tanzania (TRC), limepanga kufanya tathmini kwa ajili ya ufunguaji wa njia zilizokuwa zimefungwa ili kujua gharama za ukarabati.

Maeneo ya reli yatakayohusika ni pamoja na Kilosa – Kidatu na Manyoni – Singida.

Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mwita Waitara, aliyasema hayo jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Singida Mashariki (CCM), Miraji Mtaturu.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji serikali haioni umuhimu wa kumuenzi Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, kwa kuifanyia haraka reli ya kati kipande cha kutoka Manyoni hadi Singida ili itumike katika usafirishaji wa mizigo na abiria.

Akijibu swali hilo, Waitara alisema serikali inatambua umuhimu wa reli hiyo na wakifanya tathmini ya kujua gharama wataiboresha.

"Tunafahamu kuwa reli iliyopo ni ya zamani na tukiifanyia tathmini tutaibadilisha ili tuweke kubwa zaidi iweze kuhimili mizigo mikubwa, tunamwomba mbunge atupe muda mwaka huu mpaka mwakani utapata majibu ya ujenzi wa reli ya Singida-Manyoni ili kumuenzi Baba wa Taifa kwa kuifanyia kazi reli hii na ianze kutumika," alisema.

Katika swali la msingi, Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA), Nusrat Hanje, alihoji kwa nini kipande cha reli ya kati kutoka Manyoni hadi Singida hakipo kwenye mpango wa ukarabati.

"Je, serikali haioni umuhimu wa kukarabati kipande hicho cha reli ili kusaidia kuchochea ukuaji wa uchumi wa Mkoa wa Singida," alihoji.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Waitara, alisema wizara hiyo kupitia TRC inaendelea na mpango wa ukarabati wa mtandao wa reli iliyopo na kufufua njia za reli zilizofungwa kwa awamu kwa kuanzia na njia kuu.

"Katika kutekeleza jukumu hilo, serikali inazingatia Mpango wa Miaka Mitano wa Taifa (2021/22 – 2025/26)," alisema.

Aidha, alisema serikali itaendelea na ukarabati wa matawi ya reli ikiwamo kipande cha reli kutoka Manyoni hadi Singida kulingana na mahitaji ya ukuaji wa uchumi na uwezo wa kifedha.

"Lengo la serikali ni kuboresha miundombinu ya reli ili kurahisisha huduma za uchukuzi nchini, serikali inatambua umuhimu wa kuwapo na miundombinu ya reli imara katika kuchochea uchumi wa nchi," alisema.

Hata hivyo, alisema serikali itaendelea kufungua njia zote zilizokuwa zimefungwa ikiwa ni mkakati wake wa kurejesha huduma za usafiri wa reli wenye uhakika nchini na kuchochea ukuaji wa uchumi.

Alimuomba Mbunge na wananchi wa Mkoa wa Singida kuwa na subira wakati serikali inafanya taratibu za kufungua njia hizo.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akizungumza na Waziri wa Mambo ya Ndani, George Simbachawene, Bungeni jijini Dodoma. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

# Mbunge aomba kupelekwa vifaa tiba hospitali mpya

MBUNGE wa Mbogwe (CCM), Nicodemas Maganga, ameiomba serikali kupeleka vifaa tiba ikiwamo X-ray pamoja na vifaa vingine vya kupima wagonjwa katika hospitali mpya zilizojengwa hivi karibuni.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Festo Dugange, alisema katika mwaka wa fedha 2020/21, serikali imetoa Sh. bilioni 34 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba katika hospitali 67 za halmashauri zilizoanza kujengwa katika mwaka wa fedha 2018/19.

Alisema fedha hizo zimepelekwa Bohari Kuu ya Dawa na taratibu za kupeleka vifaa tiba katika hospitali 67 zinaendelea.

"Katika mwaka wa fedha 2019/20, serikali iliipatia Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe Sh. milioni 500 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa hospitali mpya ya halmashauri," alisema.

Aidha, alisema mwezi Mei 2021, serikali imeipatia Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe, Sh. bilioni moja kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa hospitali na majengo mapya matano yatajengwa.

"Katika mwaka wa fedha 2021/22, serikali imetenga Sh. milioni 300 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa hospitali na Sh. milioni 487 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa na vifaa tiba katika Hospitali ya Wilaya ya Mbogwe," alisema.

# Mradi kuchakata gesi kuwa kimiminika kuanza 2023

SERIKALI inatarajia kuanza ujenzi wa mradi mkubwa wa kimkakati wa kuchakata gesi kuwa katika kimiminika (LNG), ifikapo mwaka 2023, utakaogharimu Dola za Marekani bilioni 30.5.

Naibu Waziri wa Nishati, Stephen Byabato alitoa kauli hiyo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Mtwara Vijijini (CUF), Shamsia Mtamba.

Katika swali lake, mbunge huyo alisema serikali ilikuwa na mpango mzuri juu ya uwapo wa nishati ya gesi asilia nchini, lakini mpaka sasa kumekuwa na sintofahamu ya mwendelezo wa uwekezaji wa miradi hiyo ikiwamo gesi ya Mkoa wa Mtwara.

"Nini kauli ya serikali juu ya mwendelezo wa miradi hii nchini," alihoji.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Byabato, alisema serikali kupitia Shirika la Maendeleo ya Petroli nchini (TPDC), tayari imelipa fidia ya Sh. bilioni 5.71 na mradi huo unatarajiwa kukamilika ifikapo Juni, 2028.

Alisema serikali kupitia TPDC inaendelea na uwekezaji katika sekta ya rasilimali ya gesi asilia nchini kuanzia shughuli za utafutaji, uchorongaji na uendelezaji wa shughuli hizo.

"Hadi sasa takriban mikataba 11 ya utafutaji na uchimbaji wa gesi asilia inaendelea kufanyiwa kazi kati ya kampuni mbalimbali za uwekezaji kwa ushirikiano na serikali kupitia TPDC," alisema.

Alieleza kuwa hadi sasa gesi iliyogunduliwa imefikia futi za ujazo trilioni 57.54 na sehemu ya gesi hiyo hutumika katika kuzalisha umeme kwa asilimia zaidi ya 50 ya umeme wote nchini, viwandani, majumba na magari.



Nipashe

# TESA

Jumanne Juni 29, 2021

TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 14

## Haki, uhuru wa maoni ndiyo afya ya demokrasia



Ukurasa 12

Wanahabari wanatamani kuwapo kwa enzi mpya



Ukurasa 13

Ni zama za utekelezaji ajira zenye staha

TEKNOLOJIA

**NA MWANDISHI WETU**

# Afya mazingira unapoanzia gari V8

• Kuiondoa rasmi barabarani ifikapo 2022

SUALA la uharibifu wa mazingira na jitihada za kupunguza joto duniani limeanza kuchukua sura mpya baada ya kampuni ya magari kutangaza nia ya kusitisha uzalishaji wa gari maarufu la kifahari aina ya Toyota V8.

Inaeleza kuwa mzalishaji wake ameshatangaza kusitisha kuyatengeneza mwaka ujao ambayo hadi sasa hapa nchini yanatumiwa na vigogo na viongozi wa serikali.

Uamuzi huo ambao upo kwenye taarifa za mitandaoni na baadhi ya wateja walioagiza magari hayo kutoka nchini Japan, unatajwa kuwa unachukuliwa kutokana na matatizo mbalimbali yakiwamo ya kimazingira na kiufundi.

Jarida la Forbes katika moja ya makala zake zilizoelezea usitishwaji huo, zilisema sababu mojawapo ni mazingira.

Linasema ni kwa mataifa mengi kama ya Ulaya na Marekani yanapiga kampeni za kutaka kwa asilimia zote wateja kuendesha magari yanayotumia umeme au gesi badala ya petroli ili kupunguza ongezeko la joto duniani.

Magari hayo maarufu kama 'mashangingi' hutumia petroli na ulaji wake wa mafuta ni mkubwa yakitajwa kuwa kwa wastani hufuja lita moja kwa umbali mfupi wa kilometa nne au tano.

Kwa hiyo safari ya kutoka Dar hadi Arusha yenye umbali wa kilometa 700 inaweza kugharimu Shilingi takribani 400,000 za kununulia nishati.

Sababu nyingine zinazotajwa kuwa ni za kiufundi zinahusishwa na mfumo wa muundo wa gari hizo, kwa mfano ukitolewa kifaa cha kuongeza mwendo kasi kinachoitwa 'accelerator' ambacho watengenezaji wake, wanasema ni eneo linalohitaji maboresho zaidi.



Ubora wa magari una vigezo vingi lakini kimojawapo ni uwezo wa kuhimili mapito ya barabara mbovu. **PICHA: MTANDAO**

Magari yakiwa na changamoto za kiufundi mara nyingine wateja wanalazimika kumrudishia mtengenezaji kwa ajili ya maboresho jambo ambalo si afya kibiashara.

Hata hivyo, mitandao inaeleza kuwa mzalishaji wa mashangingi hayo ameandaa toleo jipya ambalo litachukua nafasi ya magari hayo ya jamii ya V8 na Lexus.

Ili kufahamu zaidi masuala ya magari hayo, Nipashe inazungumza na Mhadhiri wa Chuo cha Usafirishaji (NIT) cha Dar es Salaam Michael Kyando, anayeanza kueleza dhana ya jina la V8.

"Ni magari yenye mpangilio wa silinda zinazounda injini zinazowekwa kwa umbo la V kwa mfano V 6, 8 na nyinginezo ndiyo asili ya jina hilo ...."

Anaeleza kuwa mpangilio huo ni masuala ya uhandisi na utaalamu wa magari.

Akizungumzia zaidi kuhusu kuyaondoa kwenye soko anasema suala la mazingira hasa kuondoa nishati zinazozalisha moshi ndilo linaweza kuwa sababu kubwa ya kusitisha uzalishaji huo ili kubuni lilolo bora zaidi.

"Tunasema kitaalamu kutengeneza 'gari la hybrid' lenye mifumu ya kisasa ya injini inayotumia nishati zaidi ya moja, kama umeme au gesi," anasema.

Anasema kutokana na uzoefu wake kwenye magari mara nyingi wazalishaji viwandani wanatazama uuzaji wa magari mitumba (used) ili kuzalisha mengine mapya.

Mtaalamu huyo wa magari anasema kuwa gari kama V8 ni la kifahari na ghali hivyo pengine inawezekana kasi ya kuyauza 'used' inapungua hivyo kiwanda kinaweza kukosa oda za magari mapya, ndiyo sababu ya kuanza kujipanga upya.

**VIPI SERIKALINI?**

Tanzania ni miongoni mwa mataifa yanayotumia magari hayo jamii ya V8 na Lexus yakiitwa 'mashangingi' na pengine inaweza kuathiriwa na usitishwaji huo, ambao unaelezwa utakuja na gari kali zaidi ambalo linaweza kuwa ghali zaidi.

Nipashe, ilimuuliza Kyando ni vigezo vipi vinavyoweza kutumiwa na serikali na taasisi nyingine katika kununua gari na kupunguza gharama za uendeshaji wa sekta ya usafiri na usafirishaji.

Akijibu swali hilo, anakiri kuwa V8 ni gari la kifahari lenye gharama kubwa na hata utumiaji wake wa mafuta ni mkubwa takribani lita moja kwa kilometa nne, lakini akasisitiza kuwa katika kununua magari kuna vigezo vinavyofuatwa.

Anavitaja baadhi kuwa ni mosi linakarabatika au kutengenezeka endapo litaharibika? Vipuri vipo vya kutosha, vina ubora unaokidhi viwango, kuna mafundi wa kulitengeneza likiharibika?

Suala jingine ni lina waranti wa muda gani, upatikanaji wake kuna 'dila' au mawakala wa kampuni wanaouza magari hayo nchini ambao pia ndiyo wanaoyatengeneza na kuyasimamia yakiwa na matatizo.

Kigezo kingine ni lazima iwe aina ya gari inayopita bila matatizo kwa misimu yote kwenye barabara za vumbi, zenye mashimo na zenye matope wakati wa mvua kwa sababu sehemu kubwa ya maeneo ya vijijini hayana barabara za lami.

ELIMU

NA RAHMA SULEIMAN, ZANZIBAR

# Wanahabari wanapotamani kuwapo kwa enzi yao mpya



Baadhi ya wadau wa habari wakijadili kuhusu muswada wa sheria ya habari Zanzibar unaohitaji kufanyiwa marekebisho. **PICHA: RAHMA SUELIMAN**

WADAU wa habari Zanzibar wanataka marekebisho ya muswada wa sheria ya habari ili iendane na wakati kwa vile iliyopo ni ya muda mrefu inayohitaji mapitio na kuboreshwa ili kulinda na kujenga taaluma hiyo.

Ili kufikia azma hiyo wadau hao wamewasilisha mapendekezo yao kwenye Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar ambaye ni Msemaji Mkuu wa Serikali ili kuweza kufanyiwa kazi.

Wanachopendekeza katika muswada huo ni sheria ya kufuta usajili wa magazeti, wakala wa habari na vitabu namba 15 ya mwaka 1988 na marekebisho yake namba 8 ya mwaka 1997 na kutunga sheria ya huduma za habari na mambo yanayohusiana na hayo ya mwaka 2021.

Miongoni mwa mapendekezo yaliyopendekezwa na wadau wa habari katika sheria hiyo, wanataka mrajisi kupewa mamlaka kamili ya kusajili vyombo vya habari kwani yapo malalamiko mengi kukwama usajili wa vyombo vya habari vya binafsi Zanzibar.

Muswada huo ambao umebeba miongozo na maazimio ya habari kikanda, kimataifa pamoja na mazingira ya Zanzibar, umekamilika

> “Sisi tunataka kuweka mazingira bora ambayo waandishi wa habari yatawawezesha kufanya kazi kikamilifu kwa kushirikiana na serikali kuona mafanikio ya kuleta maendeleo yanafikiwa.

na tayari umeshakabidhiwa serikalini.

Dk. Mzuri Issa, Mkurugenzi wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar , anasema muswada huo ukibadilika na kuwa sheria utafuta sheria namba tano ya magazeti ya mwaka 1988 na vifungu vya sheria vingine ambavyo vimepitwa na wakati na pia havitoi mazingira wezeshi kwa sekta ya habari kufanyakazi kikamilifu.

“Uandishi wa habari ni kada muhimu katika kukuza na kuendeleza maendeleo ya nchi ikiwamo demokrasia, uwazi, uwajibikaji na shughuli za kiuchumi, hivyo hawanabudi kutekeleza majukumu yao chini ya mfumo bora wa sheria ambao unaendelea kuwalinda,” anasisitiza Mzuri.

Suala la kuwa na sheria ya habari mpya na bora limekuwa katika mchakato na kupitia hatua mbalimbali zilizochukuliwa zilizohusisha ukusanyaji wa maoni ya wadau hivyo muswada huo umeshirikisha fikra na maoni tofauti, anasema Mzuri.

Anasema hakuna gazeti linalomilikiwa na watu binafsi Zanzibar licha ya kuwepo kwa maombi mengi ya wawekezaji kutaka kufanya usajili yote hayo yanatokana na vikwazo vilivyopo katika sheria.

Mhadhiri wa Chuo cha Uandishi wa Habari (SUZA) Imane Duwe, anasema lengo la serikali ni kupata sheria ambayo itawawezesha waandishi wa habari kutekeleza majukumu yao vizuri.

‘’Sisi tunataka kuweka mazingira bora ambayo waandishi wa habari yatawawezesha kufanya kazi kikamilifu kwa kushirikiana na serikali kuona mafanikio ya kuleta maendeleo yanafikiwa,” anasema.

Aidha, Ofisa Mwandamizi wa Baraza la Habari Tanzania Ofisi ya Zanzibar (MCT), Shifaa Said Hassan, anaona kuwa mapendekezo yote yaliyofanywa katika sheria mpya ya mwaka 2021 lengo lake ni kutambua na kuifanya kazi ya uandishi wa habari kama ni taaluma inayotambulika na kuheshimika.

Anasema endapo sheria hiyo itafanyiwa marekebisho taaluma ya kuandika habari itaheshimiwa na kuepuka ubabaishaji unaofanywa na watu wanaojipenyeza katika kazi hiyo na mara nyingine kusababisha upotoshaji.

Anasema miongoni mwa mapendekezo ambayo yametolewa katika sheria hiyo mpya ni kumtambua mwandishi wa habari kuwa ni yule mwenye elimu kuanzia stashahada.

‘’Mapendekezo ya sheria mpya ya mwaka 2021 ya kutunga sheria ya huduma za habari lengo lake kubwa kuitambua taaluma hii rasmi na kuepuka ubabaishaji unaofanywa na watu wachache kiasi ya kuivuruga taaluma hiyo na kuonekana kila mtu anaweza kuwa mwandishi wa habari,’’ anasema.

Akizungumza katika maadhimisho ya Siku ya Uhuru wa Habari Visiwani Zanzibar, Kaimu Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Lela Mohamed Mussa, anasema serikali imeyapokea mapendekezo hayo na hatua inayofuata ni kuyapitia na kuyapeleka mbele kwa wataalamu ya makatibu wakuu kwa hatua nyingine.

Makamu wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdullah, anasema kuwepo kwa uhuru wa habari kunasaidia kujenga demokrasia ya kweli ambayo inaimarisha utawala bora, uwazi na uwajibikaji na kutokuwapo kwa uhuru wa habari kunamaanisha kukandamizwa kwa demokrasia ambayo ni kichocheo cha maendeleo, haki na uwajibikaji.

“Nchi nyingi ikiwamo Tanzania zinafahamu umuhimu wa uhuru wa habari na ndiyo maana pamoja na katiba ya Zanzibar kifungu cha 18 zimeelezea kwa kina dhana na umuhimu wa uhuru wa habari.”

Aidha, anasema kuwa baadhi ya waandishi wa habari katika nchi nyingi wamechochea balaa na kusababisha maafa yasiyosahaulika hivyo anawasisitiza waandishi kufanya utafiti na kuhakikisha wanatoa habari sahihi.

Anaeleza kuwa kumekuwa na upungufu katika kufuatilia habari za makundi yaliyo pembezoni na za vijijini, kwa vile wengi wa waandishi wamejikita zaidi katika kuandika taarifa za mijini na kuyaacha makundi mengine ambayo hayana sauti katika vyombo vya habari yakikosa huduma hiyo.

Makamu wa Pili wa Rais anawataka waandishi wa habari kufuata kwa kina maadili ya kazi zao na kuhafamu dhima na dhamana yao kwa jamii na taifa kwa ujumla akisema Serikali ya Zanzibar inathamini juhudi za sekta ya habari katika kuleta ufanisi na maendeleo hivyo serikali itaendelea kushirikiana na waandishi wa habari na kuondoa vikwazo vya upatikanaji wa habari katika taasisi za serikali.

Mwishoni mwa mwaka jana akiwaapisha mawaziri Rais wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi, aliwataka mawaziri hao kushirikiana na wadau mbalimbali na kama kuna sheria kandamizi kukaa pamoja kuzifanyia marekebisho.

ELIMU

**NA MWANDISHI WETU**

# Ni zama za utekelezaji ajira zenye staha

• Mavazi duni, ubaguzi kazini kukoma

MAVAZI unayovaa ni kama barua licha ya kuwa iko ndani ya bahasha ni lazima kila anayeliona jina juu alisome, afahamu inakwenda kwa nani. Ni kwa nadra mtu akaona bahasha akaacha kutazama kilichoandikwa.

Ndivyo mavazi yanaweza kufananishwa na bahasha iliyomfunika mtu ndani ni lazima kuiangalia. Na mara nyingi gumzo la kuvaa mavazi yanayodhalilisha hasa wanawake halikosekana kwenye jamii lakini ni kwa nadra jamii hiyo ikazungumzia mavazi ya wahudumu wa baa au 'baamedi' au hoteli ndogo na za nyota tano.

Wafanyakazi wengi kwenye eneo ni wanawake wanaovalia mavazi mafupi, ya kuwabana na wakati mwingine yanayoonyesha miili yao. Pale wanapovaa suruali nazo zinawabana na kuchora maumbile yao.

Maswali yanabaki ni lazima kuvaa nguo zinazodhalilisha? Ndizo taratibu za kuhudumu kwenye baa, hoteli, kumbi za disko na casino?

Baadhi ya wahudumu wanaofanya kazi hoteli za nyota tano wanasema ni utaratibu kwa vile wanapewa sare ambazo ni fupi, za kukubana na hutakiwa kuvaa viatu virefu na kutembea kwa mbwembwe kuvutia wateja.

Wanasema ni kama kanuni hata unapoajiriwa unaona wenzako wanachovalia na namna wanavyokupokea, unafahamu kuwa ndiyo hali halisi na kama hauko tayari unaondoka.

Kwa upande wa casino wahudumu wake wanasema ni utaratibu kuvaa mavazi yanaonyesha zaidi mwili badala ya kuusitiri na wanaofanya hivyo wameridhia na wanafurahia.

Kwenye baa na hoteli za mitaani wahudumu wanakiri kuwa hakuna anayelazimisha mfanyakazi kuvaa nguo zinazowadhalilisha ila ni maamuzi yao wenyewe, pengine kutokana na mazoea.

Meneja wa baa moja iliyoko Shekilango Dar es Salaam, anasema hakuna anayemlazimisha muhudumu kuvaa mavazi yanayombana, yaliyochanwa au kuonyesha mwili wake ni maamuzi yao wenyewe.

"Kuna baa zenye sare lakini nyingine hazina. Kinachokubalika ni rangi iwe shati nyeupe na suruali au sketi ya bluu, nyekundu au nyeusi. Hatulazimishi watu kuvaa nguo fupi, hakuna anayevaa mavazi ya kujiheshimu akaambiwa ayavue..." anasema meneja jina na baa vinahifadhiwa.

Anaeleza kuwa mara nyingi mabinti ndiyo wanaamua kuvaa nguo ndogo na fupi na wengine kutumia vipodozi vyenye zebaki au mkorogo kuchubua ngozi zao lakini si maelekezo ya waajiri.

Winfrida Daniel Meneja wa baa ya Engo iliyoko Mabibo anasema hakuna anayelazimishwa kuvaa nguo zinazomwondolea heshima ila kwenye baa kila mmoja ana uhuru wa kujiamulia.



Afya na usalama kazini ni muhimu kwa ajili ya ustawi wa wananchi na uchumi wa taifa. **PICHA: MTANDAO**

**KUKOSA MIKATABA**

Licha ya baa kuwa vitega uchumi vinavyoonekana kila mahali na pengine vyenye faida, wafanyakazi wake hawana mikataba ya ajira, hawachangii mifuko ya jamii wala kodi ya mshahara (PAYE).

Akizungumzia suala la mikataba, Winfrida, anasema wafanyakazi wa baa hawana mikataba kwa sababu wengi hawana nia ya kufanyakazi muda mrefu ni kama daraja la kuendelea kusaka kazi nyingine.

"Malipo yao si makubwa na wakati mwingine biashara hakuna. Tuseme nyakati hizi pombe zinauzwa kuanzia jioni asubuhi hakuna biashara. Ni wachache wanaokunywa soda na maji kwenye baa hazina pesa pia," anasema meneja huyo.

Anasema baa nyingi zilizo maeneo ya Mabibo zinawategemea wafanyabiashara wa soko la Mabibo au mahakama ya ndizi lakini hakuna wateja wa uhakika muda wote.

Akioongelea suala la watumishi kukosa mikataba ya ajira na stahiki kama bima ya matibabu, hifadhi ya jamii na malipo ya fidia kama wanaumia kazini, Meneja wa baa iliyoko maeneo ya Mlimani City (jina tunalo), anasema ni vigumu kukubali kukatwa fedha zao.

"Mishahara si mikubwa ni kama Shilingi 100,000 hadi 120,000 unapoanza mjadala wa mkataba na makato hawako tayari. Hata kama, ukimwambia unahitaji bima ya matibabu ili kujihudumia ukiumia hasa kwa vile utakuwa hufanyikazi hawezi kukubali." Anasema meneja huyo.

**AJIRA ZA STAHA**

Licha ya maelezo ya utetezi leo hii dunia inasisitiza kazi zenye staha zisizo na udhalilishaji, zenye mikataba ya ajira, hifadhi za jamii, pensheni uzeeni na bima za matibabu.

Shirika la Kazi la Umoja wa Mataifa (ILO), linahimiza mataifa na waajiri kuthamini utu wa wafanyakazi na kuwapa stahiki zao kwa haki na kuondoa unyanyasaji wa aina zote kazini.

Mkataba Namba C 190 wa ILO ndiyo unaowalenga walio katika ajira, wanaziotafuta, walio kwenye mafunzo kazini, walioachishwa, wanaojitolea pamoja na waajiri wao, kuthaminiwa utu wao.

> "Hata kama, ukimwambia unahitaji bima ya matibabu ili kujihudumia ukiumia hasa kwa vile utakuwa hufanyikazi hawezi kukubali.

Lengo la C 190 linatajwa na ILO kuwa ni kufutilia mbali ukatili na unyanyasanyi kazini kwa kuwahakikishia watu ajira zinazoheshimu utu na kuthamini ubinadamu.

Kwa mujibu wa ILO mkataba wa C 190 umeangazia kuhusisha ulinzi kwa wote wanaohusika na kazi au ajira, iwe ya mkataba, kujitolea na kile aliyeko sehemu za kazi.

Mkataba huo ulioanza kutekelezwa mwezi huu ni mlinzi wa mambo ya msingi yanayohusu ustawi na heshima ya mfanyakazi bila kujali ameajiriwa sekta rasmi au isiyo rasmi.

ILO inawaagiza wanachama wa UN ikiwamo Tanzania kuusaini, kuridhia na kuutekeleza kwa kutunga sheria na kuzisimamia kwa mujibu wa taratibu, miongozo na sheria za kazi ili kulinda utu wa mtu.

Mkataba huo unataka kuondoa aina zote za ubaguzi na unyanyasaji kazini yakiwamo mavazi mafupi, yanayoonyesha maumbile ya wanawake, malipo kiduchu, unyanyasaji kingono ili upate kazi na ubaguzi.

Aidha, unataka kuondoa unyanyasaji kingono, kijinsia, kukandamiza wanawake na kuondoa kila aina ya ubaguzi wa kiajira baina ya wanawake na wanaume.

Hata hivyo, wafanyakazi wengi nchini hawaufahamu wakiwamo wanawake walio kwenye baa, hotelini na maeneo ya burudani ambao wengi wananyanyaswa na kudhlilishwa kingono, kijinsia na kiajiriwa kwa kulipwa ujira kiduchu, jambo linalohitaji kuutangaza.

Akizungumza na wanawake mkoani Dodoma hivi karibuni, Rais Samia Suluhu Hassan, alisema wanawake wengi ndiyo walioko kwenye ajira zisizo rasmi.

Kwa mujibu wa Rais Watanzania takribani 3,000,000 wenye ajira rasmi wanawake ni milioni moja idadi ambayo inaonyesha kuwa wengi hawajaajiriwa licha ya kwamba ndiyo wengi zaidi wakiwa ni asilimia 51 ya Watanzania wote.

Kwa hiyo ni vyema Tanzania kuridhia mkataba huo na kuwahamasisha waajiri kuutekeleza ili kinamama waepushwe na kufanya kazi zisizo na staha, zisizo na mikataba, wasinyanyaswe na pia wapewe stahili muhimu kama likizo zenye malipo, livu za uzazi na kuthaminiwa utu wao.

ELIMU

NA MWANDISHI WETU

# Haki, uhuru wa maoni ndiyo afya ya mtazamo



Serikali, vyombo vya dola na raia ni wadau wakuu kwenye utii wa sheria, usimamizi wa haki na ulinzi wa utu na heshima ya watu. **PICHA: MTANDAO**

HAKI ya kutoa maoni na uhuru wa kujieleza vimerejeshwa. Watu wanapumua sasa. Ni kwa sababu kwa miaka mitano iliyopita uhuru huo ulikufa, hakukuwa na kukosoa serikali au taasisi ya dola.

Lakini baada ya siku 100 za uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan, misuli ya kupumua inafanyakazi.

Ni maoni ya Mwenyekiti wa Kamati wa Kitaifa ya Maaskofu na Mashekhe ya Maadili, Amani na Haki za Bindamu kwa Jamii ya Madhehebu ya Dini nchini, Askofu William Mwamalanga.

Anasema hayo akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam, akirejea namna ambavyo watu wengi walinyamaza kuanzia watu binafsi, viongozi wa dini na wasiasa kwa kukosa uhuru wa maoni.

Mwamalanga anakumbusha kuwa viongozi wa dini walinyang'anywa pasi za kusafiria baadhi wakidaiwa kuwa si raia na hilo linatokea pale mtu anapotoa neno dhidi ya maamuzi ya serikali na huo ulikuwa ndiyo wakati wa kuchunguzwa urai.

Askofu huyo anazitaja siku 100 za Rais Samia kuwa zimerejesha uhuru, utu, haki na amani tunu ambazo kama mshumaa zilizimwa na awamu ya tano.

"Hakika ndani ya siku 100 Rais Samia amefanya mambo makubwa bila uwepo wa katiba mpya, hili linatufundisha kuwa uongozi wa nchi unahitaji kiongozi siyo mtawala," anasema.

Anafananisha ukosefu wa uhuru wa maoni na kazi ya kutengeneza raia wanyonge na umaskini kwani kwa haraka wananchi walinyimwa uhuru wa kuhoji, kukosoa na kujitetea, mbele vyombo vya kutoa haki kwani vyote vilikuwa vinafanya kazi kwa hofu.

Anasema jambo hilo liliondoa ustawi kwenye maamuzi mbalimbali na kusababisha kukua kwa kundi la watu au viongozi wanaoogopwa na lakini pia jingine la wenye hofu na wasiojiamini.

**KUKEMEA WABADHIRIFU**

"Vyombo vya habari ambavyo vinatajwa kuwa jicho huru navyo havikuugusa ukweli. Hata vilishindwa kufichua dhuluma ufisadi na uonevu mwingine ndani ya jamii."

Anasema vyombo hivyo vilishindwa jukumu la kuisaidia serikali na matokeo yake wapo wachache waliojitokeza kupora mali za umma na za serikali kama ilivyoshuhudiwa kwenye taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali -CAG ya mwaka 2019/2021.

Anasema siku 100 za Rais ni somo kuwa nafasi za uongozi wa juu zisiwe nafasi za mihemuko ya kivyama vya siasa.

> "Usajili wa makanisa na misikiti unachukua miaka mingi kupata cheti cha usajili, wakati nchi za Afrika Mashariki na Afrika nzima usajili huo ni siku tatu hadi saba.

Ni muhimu katiba ya nchi kutumiwa na mamlaka ili madaraka yatoke kwa wananchi na si kwa viongozi.

Anaendelea kusema kuwa katika siku 100 za Rais Samia, waliotoa maoni yao na kujieleza kile walichodhani kinahitaji kuboreshwa wamepewa haki yao.

"Wakulima wamelipwa stahili zao, makandarasi na wafanyakazi wamelipwa. Wanafunzi wa mikopo ya elimu ya juu pia wamesikilizwa. Hili linawezekana kwa kuwa nchi imepata kiongozi anayesimamia haki na misingi ya katiba na sheria."

**VIONGOZI WA DINI**

Mwamalanga, anasema kukaa kimya hakusaidii na wakati mwingine ni lazima kusema.

"Siachi kuwapongeza maaskofu wenzangu ambao awamu ya tano 'iliwatumbua' na kuwanyang'anya pasi za kusafiria na wengine kutishiwa. Leo wako huru wanaendelea kuhubiri Injili," anasema na kumpongeza Rais kwa kuleta suluhu na kuongeza kuwa taifa litapata maendeleo kiuchumi, kisiasa na kwenye uhuru wa kuabudu pia.

Aidha, anataka haki na utawala wa sheria viendelee, akiungana na Baraza la Maaskofu Katoliki (TEC) kumuomba Rais kuangalia sheria kandamizi kwenye taasisi za kidini ili wananchi wafikiwe na huduma za kijamii bila vikwazo.

Anasema kuzibana taasisi za kidini kwa sheria kunakwamisha jamii na wananchi kupata huduma, kwa sababu taasisi hizo ni njia ya haraka ya kuwafikia wananchi.

"Tunakuomba uondoe kero ya usajili wa taasisi hizi kwa kuunda chombo cha usajili kama ilivyo kwenye vyama vya siasa," Anasema.

"Usajili wa makanisa na misikiti unachukua miaka mingi kupata cheti cha usajili, wakati nchi za Afrika Mashariki na Afrika nzima usajili huo ni siku tatu hadi saba."

Anasema kusajili taasisi za dini kwa miaka mingi kunaweza kutafsiriwa kuwa ni agenda ya kuminya uhuru wa kuabudu ambao upo kikatiba.

Wakizungumzia suala la kurejesha uhuru wa maoni na kujieleza wanafunzi wa Taasisi wa Ustawi wa Jamii ya Dar es Salaam, wanasema ni muhimu kuurejesha kwa vile watu waliingiwa na hofu sana.

Amri Semu, mwanafunzi wa mwaka wa pili, anasema kukosekana haki ya maoni na uhuru wa kujieleza kunaondoa amani, kwa vile muda wote hofu inatanda hivyo kuogopa kusema ukweli.

Semu akizungumzia vyombo vya habari, anasema wakati mwingine vilikosa wateja hasa magazeti ambayo yalikosa wasomaji. Mwanafunzi mwingine Happiness Minja, anasema kukosekana uhuru wa maoni na kujieleza kunaua matumani.

"Matumaini yakifa huondoa amani, uhuru na ari ya kujituma kupata maendeleo kwa sababu raia wanaogopa. Ni vigumu kusema ukweli, kuwa na utaifa na uzalendo kwa sababu serikali inatamani watu wote wahubiri na kufundisha kile inachokisema.

Happiness anasema kuwapo uhuru wa maoni na haki kwa raia na kuondoa sheria kandamizi ni njia sahihi ya kupata maendeleo kwa vile huo ndiyo utaratibu wa kuondoa uonevu kwa kuwa sheria hazitumiwi, kukandamiza, kuonea na kuumiza raia.





# Machinga wataka washiriki kwenye kufanya maamuzi

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

UMOJA wa wafanyabiashara wadogo Mkoa wa Dodoma, umeziomba Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini, washirikishwe wanapofanya maamuzi kuhusu wao, ili kuepukana na migogoro isiyo ya lazima.

Rai hiyo ilitolewa na Mwenyekiti wa umoja huo, Bruno Mponzi, alipokuwa akizungumza kwenye kikao cha pamoja kati wafanyabiashara hao na uongozi wa Jiji la Dodoma.

"Kuna wakati zinatokea sintofahamu kutokana na viongozi kwenye Majiji, Halmashauri, Mji na Manispaa kufanya maamuzi kwa kutowashirikisha wafanyabiashara kwenye maamuzi," alisema Mponzi.

Alisema ili tofauti hizo ziepukike inahitaji mambo matano muhimu ya ushirikishwaji, ambayo ni pamoja na utolewaji wa taarifa za operesheni ya uhamasishaji zitolewe mapema kadhalika na elimu ya kutosha pindi halmashauri, majiji na manispaa wanapotaka kuwahamisha machinga, ili kusiwapo na migogoro isiyo na tija.

Alitaja hatua nyingine ambayo inayohitaji kwa machinga hao ni kwenye maeneo kunakotakiwa kuwa mazingira rafiki kwenye miundombinu kwa wateja wao.

Mponzi alisema mambo hayo yakizingatiwa kamwe kwa upande wa machinga hawawezi kuwa na misuguano ikiwa watashirikishwa kwa pamoja na kuwataka machinga kuhakikisha wanafuata kanuni na sheria zilizopo, ili kuepuka malalamiko isiyokuwa na tija kwa mfanyabiashara wadogo.

Alisema baadhi ya machinga wamekuwa wakikiuka kanuni na sheria na kujikuta wakifanya biashara zao bila utaratibu na hatimaye kujikuta wakikwamishwa kufikia malengo yao.

Ofisa Masoko wa Jiji la Dodoma, Erick Matiku, aliwataka machinga kuzingatia kanuni ikiwamo na muda wa kufanya biashara zao, kwenye maeneo waliyotengewa ikiwamo barabara ya Nyerere Square.

# COSTECH yataka kulindwa kwa shoroba

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TUME ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), imesema ipo haja ya kulinda shoroba za wanyamapori, ili kujiepusha na mwingiliano wa wanyama hao na binadamu.

Mkurugenzi wa Menejimenti ya Maarifa wa COSTECH, Dk. Philibert Luhunga, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipokuwa akijibu hoja kutoka kwa Dk. Cecilia Lweri wa Taasisi ya Wanyamapori nchini (TAWIRI), kwenye warsha iliyoandaliwa na tume hiyo, kuhusu watafiti kutoka taasisi mbalimbali nchini.

Alisema migogoro kati ya binadamu na wanyamapori inahusishwa sana na mabadiliko kwenye idadi ya watu, uchumi, hali ya hewa na mifumo ya matumizi ya ardhi na kiteknolojia.

Aidha alisema kwa Tanzania migogoro hiyo imekuwa ikichochewa na ongezeko la idadi kubwa ya watu, inayokwenda sambamba na kuongezeka kwa mahitaji ya matumizi ya ardhi.

"Ifike wakati sasa jamii ipewe elimu kuhusu shoroba za wanyamapori, ili kuepuka madhara yanazoweza kujitokeza pindi wanyama watakapopita maeneo wanaoishi jamii," alisema Dk. Luhunga.

Dk. Leweri kutoka TAWIRI alisema migogoro kati ya binadamu na wanyamapori imesababisha hasara kubwa za kijamii, kiuchumi na kuathiri uhifadhi wa wanyamapori kwa kuingilia makazi yao.

Alisema ushahidi wa kiufuatiliaji unaonyesha kwamba kuna shoroba za wanyamapori ambazo bado zinafaa kwa matumizi ya wanyamapori zinazopita katika ardhi za vijiji na zikitumika kwa shughuli mbalimbali, ikiwamo makazi, kilimo na ufugaji.

Alibainisha kukithiri kwa migogoro hiyo kunachangiwa zaidi na hali ya umaskini na ukosefu wa teknolojia na utekelezaji duni wa malengo ya kisekta na kwamba sera zote zinazohusiana na matumizi ya ardhi ziunganishwe, ili zizungumze pamoja kuhusu masuala yote ya matumizi hayo.

Dk. Leweri alisema ikifanyika hivyo, itasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza au kutokomeza kabisa migogoro baina ya jamii na maeneo ambayo wanyamapori wanapita kila baada ya msimu fulani.

Alisema idadi ya wanyamapori iliyoongezeka imesababisha mahitaji ya maeneo mengine mapya ya makazi ya wanyamapori na hivyo kurudi katika makazi yao ya zamani.




Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Medical Research International (HJFMRI), Sally Chalamila, akizungumza na waandishi wa habari (hawapo pichani), kwenye maadhimisho ya kitaifa ya Siku ya Kupiga Vita Dawa za Kulevya nchini kuhusu ushirikiano uliopo baina yao na serikali katika mapambano ya kudhibiti dawa za kulevya nchini, yaliyofanyika viwanja vya Nyerere Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Maofisa utumishi wakumbushwa wajibu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imewataka maofisa utumishi, kutimiza wajibu wao kwa kufuata sheria na miongozo, ili kuleta ufanisi kwenye majukumu yao.

Mkurugenzi wa Uendeshaji Sera wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Agnes Kisaka, aliyabainisha hayo jana kwenye Mkutano Mkuu wa Chama cha Maofisa Utumishi na Maofisa Utawala (THRAOT), kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mohamed Mchengerwa.

Alisema kila ofisa utawala na utumishi wa serikali anapaswa kutimiza wajibu wake, kwa kufuata sheria na mwongozo wa serikali, ili kusaidia kuboresha utendaji wao na kwamba wajibu wao ni kufanya kazi kwa mujibu wa sera, sheria, kanuni serikalini.

Aidha, alisema serikali inatumia fedha nyingi kila mwezi, kuhakikisha watumishi wote waliopo katika orodha ya malipo serikalini, wanapata stahiki zao kwa wakati licha ya kuwa kuna baadhi ya watumishi hawawajibiki ipasavyo.

"Hayati Benjamini Mkapa alisema tusijiulize muda gani tumetumia kufanya kazi bali tujiulize tumefanya nini kwa muda tuliopewa kufanya kazi," alisema.

Alihimiza watumishi hao kutumia chama hicho kwa kuwakumbusha wafanyakazi wote kufanya kazi kwa bidii na kwa uadilifu mkubwa pamoja na kujiepusha na vitendo vya rushwa wakati wa kutekeleza majukumu yao.

Kisaka alisema ni matumani yake chama hicho kitakuwa kiunganishi kikubwa baina ya watalaamu wa kada husika na watumishi wengine na hivyo kuwa chachu ya mabadiliko katika kazi na watumishi hao kutumia chama hicho kujitangaza kudhihirisha kuwa maofisa utumishi na tawala.

"Natarajia kuzinduliwa kwa chama hiki, itakuwa ni mwanzo wa kurejesha heshima ya taaluma hii kwa wafanyakazi na wananchi, ni kizuri, endapo mkikitumia kwa ajili ya kufanya kazi nzuri, ili kurejesha heshima yenu nchini," alisema Kasaka.



# Machinga kutoondolewa kwa sasa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI mkoani Mbeya, imesema haitawaondoa wafanyabiashara wadogo maarufu kwa jina la 'machinga' wanaofanya shughuli zao kwenye maeneo yasiyokuwa rasmi ikiwamo kwenye hifadhi za barabara mpaka itakapowaboreshea miundombinu kwenye soko la uwanja wa ndege wa zamani.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alisema wakati wa mahojiano maalumu na Nipashe na kuisema kwa sasa serikali inawaacha wafanyabiashara hao wafanye kazi zao kwa uhuru katika maeneo hayo.

Alisema serikali inaendelea na ujenzi wa miundombinu ya kisasa kwenye soko hilo la Uwanja wa Ndege wa zamani linalotarajiwa kuwa na vibanda 6,000, kuboresha miundombinu ya barabara na kituo kidogo cha daladala cha kisasa.

Alisema baada ya miundombinu hiyo kukamilika watawahamisha wajasiriamali hao kwa utaratibu maalumu na kwamba kwa sasa wafanyabiashara hao wanatakiwa waendelee na kazi huku wakijiandaa kuhama baada ya soko kukamilika.

"Kwa sasa hatuwezi kumhamisha mtu na kumpeleka eneo ambalo hata miundombinu hakuna, kipaumbele chetu ni kuhakikisha wafanyabiashara hawa hawanyanyasiki ndani ya mkoa wetu, tunataka tuboreshe miundombinu ili ndio tuwahamishe," alisema Homera.

Aliwataka wajasiriamali hao pamoja na wafanyabiashara wengine kuwa na subira wakati serikali ikiendelea kuboresha miundombinu hiyo ya soko la Machinga ambalo walikabidhiwa na aliyekuwa Rais wa awamu ya tano, Hayati Dk. John Magufuli.

Homera aliwataka viongozi wa serikali kutowanyanyasa wafanyabiashara hao na badala yake wawape elimu ya namna ya kufanya biashara zao huku wakilinda usalama wao.

Baadhi ya Machinga wa Jiji la Mbeya, waliishukuru serikali kwa uamuzi wake wa kutowaondoa kwenye maeneo hayo wakisema kwa sasa soko la Uwanja wa Ndege halijakamilika na hata wateja hawawafikii kutokana na kutokuwapo kwa magari yanayopeleka abiria.

Mmoja wa wamachinga hao, Juma Swaya alisema eneo hilo huwa linakuwa na maji mengi wakati wa mvua na vigumu kwa wateja kwenda hali inayolifanya kuwa la msimu wa kiangazi pekee.

Alisema baada ya serikali kuhamisha mabasi ya kwenda Chunya kutoka stendi kuu kwenda katika eneo hilo la Uwanja wa Ndege angalau kuna wateja wanajitokeza na kuiomba serikali kuhamisha na mabasi mengine ya kuelekea wilayani katika eneo hilo.

"Ni kweli kwenye maeneo ya hifadhi ya barabara usalama huwa ni mdogo maana unaweza ukagongwa na magari na ukizingatia sasa hivi kuna hata bajaji na bodaboda ambazo mara nyingi hazifuati sheria, lakini hatuna namna maana soko letu bado halijakamilika," alisema Swaya.

Naye Bonface Chigonya, alisema wanakimbilia kwenye maeneo ya barabarani kwa sababu ndiko kwenye wateja wengi na kwamba endapo serikali itapeleka kituo cha daladala kwenye soko la Uwanja wa Ndege hawatakuwa na sababu ya kuendelea kuuzia bidhaa zao barabarani.

Alimshukuru Mkuu wa mkoa kwa kuamua kuwatetea ili wasiondolewe kwenye maeneo hayo ya hifadhi ya barabara kabla soko lao halijaboreshwa.

Mwezi Mei 2019 wakati aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hayati Dk. Magufuli alipofanya ziara jijini Mbeya, Naibu Spika Dk. Tulia Ackson alimuomba awapatie wafanyabiashara hao eneo la Uwanja wa Ndege ili wafanyie biashara zao jambo ambalo liliridhiwa na rais na kuagiza wajengewe miundombinu.



Kamanda wa Polisi mkoani Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, (SACP) Ulrich Matei (kulia), akizungumza na abiria aliowakamata jana kwenye operesheni maalumu wakiwa wamepanda wanane kwenye bajaji moja hali inayohatarisha usalama wao. **PICHA: NEBART MSOKWA.**

# DC awaweka 'kitimoto' maofisa Mbeya-WSSA

**Na Nebart Msokwa,** BUSOKELO

MKUU wa Wilaya ya Rungwe, mkoani Mbeya, Dk. Vicent Naano, amewaweka 'kitimoto' maofisa wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya (Mbeya-WSSA) na Wakala wa Maji Vijijini (RUWASA) wa Wilaya hiyo akiwataka kukamilisha Mradi wa Maji wa Ikama Ndembo ndani ya mwezi mmoja.

Dk. Naano alitoa agizo hili mwishoni mwa wiki alipofanya ziara ya kukagua mradi huo unaojengwa na serikali kwa gharama ya Sh. bilioni moja pamoja na miradi mingine ya maji katika Halmashauri ya Busokelo na kubaini kusuasua kwa mradi huo na udanganyifu.

Alisema alibaini katika baadhi ya maeneo maofisa hao wa RUWASA waliwashawishi wananchi waseme kwamba maji yanatoka wakati kiuhalisia bado hawapati huduma hiyo kama ilivyokuwa lengo la serikali.

Alisema lengo la serikali ni kuhakikisha inamtua ndoo ya maji mwanamke kwa kusogeza huduma hiyo karibu na makazi yao, lakini alichokibaini kwenye mradi huo ni ubabaishaji unaofanywa na mamlaka hizo mbili.

"Lakini baada ya kuangalia tangi hili, tumebaini kwamba kiwango cha maji yanayoingia humu ni kidogo sana na ili maji yajae inatakiwa yafungwe kwa siku tatu ndio yaachiwe kwenda kwa wananchi, sasa nawapa mwezi mmoja hakikisheni tatizo hili linaisha na wananchi waanza kupata huduma," alisema Dk. Naano. Alisema endapo hawatatatua tatizo hilo mradi huo hautakuwa na maana yoyote kwa wananchi wa Busokelo kwa maelezo kuwa hawataweza kupata huduma ya maji kama inavyotakiwa.

Aliwataka watekelezaji wa miradi yote ya maji ndani ya wilaya hiyo kuhakikisha wanashirikiana na viongozi wa serikali wilayani humo ili miradi hiyo ifanikiwe.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Busokelo, Anyosisye Njobelo, alisema halmashauri hiyo ina vyanzo vingi vya maji, lakini watendaji wa Mamlaka zinazotakiwa kupeleka maji kwa wananchi hawana ubunifu wa namna sahihi ya kuvitumia.

Alisema endapo vyanzo hivyo vingetumika vizuri kuna uwezekano tatizo la maji katika maeneo yote ya Wilaya ya Rungwe likamalizika na ziada kupelekwa katika wilaya zingine ikiwamo Wilaya ya Kyela ambayo ina tatizo kubwa la maji.

Alisema wananchi wa wilaya hiyo ndio wasimamizi wakuu wa miradi ya maji inayotekelezwa kwenye maeneo yao na kuwataka watekelezaji wa miradi hiyo kuwashirikisha pia wananchi ili na wao wajue kinachoendelea.

"Hakuna sababu ya wananchi wa Busokelo kukosa maji safi na salama, tatizo lililopo ni ushirikishwaji unakuwa hakuna, wanajenga miradi bila kutushirikisha, wangekuwa wanatushirikisha kulikuwa na uwezekano na sisi tukatoa ushauri wa kuboresha miradi hii," alisema Njobelo.

Kaimu Meneja wa RUWASA Wilaya ya Rungwe, Paul Kambona, alisema mradi wa Ikama Ndembo unatekelezwa na Mbeya-WSSA na unatarajiwa kunufaisha wananchi wa vijiji vya Ikama na Ndemo na kwamba majina ya vijiji hivyo ndiyo asili ya jina la mradi na vipo kwenye kata mbili tofauti za Kapula na Rwangwa.

Alisema mradi huo mpaka sasa umetumia zaidi ya Sh. milioni 900 na umekamilika kwa asilimia 98 na ukikamilika utawanufaisha wananchi wasiopungua 6,000.

# Polisi yaanza operesheni maalum madereva bajaji

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya, limeanza operesheni maalumu ya kuwashughulikia madereva wa pikipiki za magurudumu matatu maarufu kwa jina la bajaji pamoja na abiria wao wanaokiuka sheria za usalama barabarani ili kupungua ajali.

Jeshi hilo linaendelea na ukaguzi wa mabasi yanayofanya safari zake kati ya jiji hilo na maeneo ya mikoa mingine ikiwa ni utekelezaji wa agizo la Kamishna Jenerali wa Jeshi la Polisi nchini (IGP), Simon Sirro la kuhakikisha mabasi yote yanakaguliwa.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi (SACP), Ulrich Matei ndiye aliyeongoza operesheni hiyo baada ya kubaini kuwa kumekuwa na ukiukwaji mkubwa wa sheria.

Alisema baadhi ya madereva bajaji wanapakia abiria wengi kuliko idadi inayokubalika kisheria na kuwa miongoni mwa vyanzo vya ajali za barabarani.

"Katika eneo la Nzovwe mimi mwenyewe nimekamata bajaji ikiwa imepakia abiria wanane, tumemkamata dereva pamoja na abiria wake tumewasweka ndani, lengo letu ni kuhakikisha tunakomesha vitendo hivi," alisema Kamanda Matei.

Alisema mbali na ukiukwaji huo wa sheria pia operesheni hiyo inaenda sambamba na kuweka mpangilio mzuri wa vyombo vya usafiri katika Jiji la Mbeya hasa kuepusha migogoro kati ya bajaji na daladala.

Vilevile, alisema katika operesheni hiyo watahakikisha madereva wote wa vyombo vya moto wanafanya kazi hiyo wakiwa na leseni na yeyote atakayebainika kufanya kazi hiyo bila leseni atachukuliwa hatua za kisheria.

## Migogoro ya ardhi 125 Kusini Unguja yapatiwa ufumbuzi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUU wa Mkoa Kusini Unguja, Rashid Hadidi Rashid, amesema jumla ya migogoro 125 ya ardhi ilijitokeza katika mkoa huo, kati yake 43 imepatiwa ufumbuzi.

Akitoa taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya kiutendaji wa mkoa huo, ofisini kwake Tunguu, nje ya Mjini wa Zanzibar, akizungumza na waandishi wa habari, alisema migogoro iliopatiwa ufumbuzi ni ya Wilaya ya Kati na Kusini Unguja.

Alisema miongoni mwa migogoro iliyokuwa ikilalamikiwa na wananchi ni pamoja na eneo moja la ardhi kumilikiwa na watu wawili tofauti.

Alisema ukosefu wa elimu kwa baadhi ya wananchi unachangia wingi wa migogoro ya ardhi kwa kutofahamu taratibu za kisheria kwa kesi ambazo zimeshatolewa hukumu na Mahakama ya Ardhi au ziko mahakamani.

Akizungumzia ufuatiliaji wa miradi mbalimbali ya kimaendeleo katika awamu ya nane ya uongozi kuanzia Desemba, mwaka jana hadi Juni mwaka huu, alisema katika Mkoa wa Kusini, jumla ya miradi minane mikubwa imo katika mkoa huo.

Alisema miongoni mwa miradi hiyo ni mradi wa ujenzi wa Mahakama Kuu Tunguu ambao hivi karibuni utakabidhishwa serikalini pamoja na Shule ya Kibuteni yenye dahalia tayari vijana 113 wanaoendelea na masomo.

Alieleza kuwa mradi wa ujenzi wa Hospitali ya Binguni, bado haujafikia kiwango kinachotakiwa kutokana na uhaba wa fedha hivyo serikali iko katika harakati za kuufanikisha.

Alisema mradi wa umwagiliaji maji wa kilimo Cheju, unaendelea vizuri na utakabidhishwa serikalini huku mradi wa shule ya Kisongo wa elimu ya ufundi, haujakabidhiwa kutokana na matatizo baina ya mkandarasi na wizara.

Alibainisha kuwa mkoa umefanikiwa kukusanya kiasi cha Sh. bilioni 700 kwa Wilaya ya Kati na Kusini imekusanya zaidi ya Sh. milioni 500 zimepatikana kwa halmashauri na mabaraza ya mjini kuanzia Desemba hadi Juni 2020/2021.

# Wakulima wa mwani walia upatikanaji wa soko

**Na Mwandishi Wetu**

WAKULIMA wa mwani kisiwani Pemba, wameiomba serikali ya Zanzibar kuingilia kati upatikanaji wa soko.

Lengo ni kuwanusuru na hali ngumu ya maisha wanayokabiliana nayo kutokana na wanunuzi kusitisha ununuaji wa zao hilo.

Hayo yalisemwa jana na wanakikundi cha Muungano kilichopo Shehia ya Makangale Wilaya ya Micheweni Mkoa wa Kaskazini Pemba, wakati wakizungumza na Mkurugenzi wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar, Dk. Mzuri Issa, alipowatembelea kukagua maendeleo ya kikudi hicho.

Haji Hamad Haji, mmoja wa wanakikundi hicho, alisema licha ya wananchi wengi Zanzibar kuhamasika kuzalisha kwa wingi zao hilo, kukosekana kwa soko, kunadumaza hali za wakulima hao.

"Ukija vijijini watu tunateseka sana na zao hili, migongo imevunjika kwa kuzalisha mwani lakini manufaa hakuna. Tumevuna mwani tumebaki kuuweka ndani kutokana hakuna wa kumuuzia," alisema Haji.

Aidha, alisema tatizo hilo linatokana na wananchi kukosa taaluma zaidi ya namna ya kusarifu mwani kwa matumizi mingine jambo ambalo linasababisha wakulima wengi kutegemea njia moja ya uuzaji bila kuwa na mbadala wake.

Kwa upande wake, Time Ismail Ali, mwenyekiti wa kikundi hicho, alisema tangu wanunuzi wasitishe kununua zao hilo ambalo kwa kiwango kikubwa linazalishwa na wanawake, imesababisha familia nyingi kukumbwa na hali ngumu ya maisha. "Kusema ukweli soko la mwani limetuathiri sana wakulima hapa Makangale hasa sisi wanawake, kwani hiki ndicho kilimo chetu na tulikuwa tukipata angalau pesa kidogo ya kujikimu na familia zetu. Hali imekuwa tofauti tangu kampuni zisitishe kununua mwani. Tunavuna sana lakini upo ndani unaoza hatuna pa kupeleka," alisema Ali.

Aidha, kutokana na tatizo hilo, alisema wakulima wengi wanakata tamaa ya kuendelea na uzalishaji jambo ambalo linazidi kuhatarisha uchumi wa familia hizo.

Aliiomba serikali kusaidia kumaliza tatizo na hali ikiendelea kuwa hivyo inahatarisha kutokea madhara zaidi kwa wananchi, ikiwa ni pamoja na njaa.

Khadija Masoud Ali, alisema licha ya kukabiliana na matatizo hayo, ukosefu wa zana bora za kuwawezesha kuzalisha ni kikwazo kwao, jambo linalosababisha kukumbana na viumbe hatarishi wanaotishia usalama wao wanapokua baharini.

"Sisi wakulima bado tunafanya kazi katika mazingira magumu, hatuna zana bora za kujilinda tunapokuwa baharini. Wakati mwingine tunang'atwa na wadudu hatarishi na kusababisha kukaa ndani miezi zaidi ya mitatu na wengine kupata ulemavu wa kudumu," alisema mwanakikundi huyo.

Dk. Mzuri Issa aliwataka wakulima hao kutokata tamaa na uzalishaji ili kujiendeleza kiuchumi licha ya matatizo yanayowakabili.

"Kikubwa tuendelee na uzalishaji tusirudi nyuma kwani ndiyo shughuli zetu, nasisi wadau tutajitahidi kuwasilisha changamoto zenu sehemu husika ili angalau ziweze kutafutiwa ufumbuzi na kilimo hiki kiweze kuwa mkombozi kwa wakulima kama mazao mengine yanayolimwa hapa Zanzibar," alisema Issa. Ziara ya Dk. Issa Kisiwani Pemba ililenga kutembelea na kukagua maendeleo ya vikundi vya wanawake wajasiriamali vinavyowezeshwa na chama hicho, kupitia mradi wa kuwawezesha wanawake Kiuchumi Zanzibar (WEZA) kwa ufadhili wa Taasisi ya Zanzibar Milele Foundation.



Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Rashid Hadid Rashid, akitoa taarifa kwa waandishi wa habari kuhusu utekelezaji wa kazi ndani ya mkoa wake kuanzia Desemba 2020 hadi Juni mwaka huu huko ofisini kwake Tunguu Wilaya ya Kati Mkoa wa Kusini Unguja. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Serikali yapaisha bei ya karafuu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar, imeongeza bei ya zao la karafuu kwa daraja la pili na la tatu, ili kuongeza thamani ya uzalishaji wa zao hilo.

Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Omar Said Shaaban, aliyasema hayo alipokuwa akitoa taarifa kwa waandhishi wa habari ofisini kwake Malindi Mjini, Unguja. Alisema Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC), linatarajia kufungua vituo vya ununuzi wa karafuu Julai 3, mwaka huu, wakati bei ya ununuzi karafuu kutoka kwa mkulima daraja la kwanza itauzwa Sh. 14,000. Alisema karafuu yenye kiwango cha daraja la pili, itauzwa Sh. 13,000 badala ya Sh. 12,000 bei ya zamani na daraja la tatu itauzwa Sh. 12,000 badala ya Sh. 11,000 hapo awali.

Aidha, alisema kuwa, ahadi ya serikali ya kununua zao hilo la karafuu bado inaendelea na itakuwa inanunua kwa asilimia 80 ya bei la soko la dunia.

"Serikali ya awamu ya nane inayoongozwa na Dk. Hussein Ali Mwinyi, imeahidi kusimamia kwa lengo la kuwapatia bei nzuri wakulima wake, ili kujipatia kipato zaidi na kuendelea kushughulikia zao hili kwa juhudi na umuhimu zaidi," alisema Shaaban.

Aidha, alisema wizara imeweka mfumo maalum wa ununuaji wa karafuu kwa njia ya mtandao, ikiwa na lengo la kupunguza vitendo vya uhalifu katika kipindi cha ununuaji wa zao hilo.

Waziri huyo aliviomba vyombo vya ulinzi na usalama, kuzidisha ulinzi ili wakulima wasisafirishe karafuu kwa njia ya magendo, na kuwataka wakulima kuzidisha uadilifu kwa kuchuma karafuu zilizo komaa pamoja na kuzianika mahali panaporuhusiwa, ili kuwa na daraja la mwanzo.

Waziri Shaaban, aliwapongeza wakuu wa mikoa na wilaya pamoja na vyombo vya ulinzi na usalama kwa kusimamia na kukabiliana na magendo yanayofanywa na baadhi ya wafanyabiashara wa karafuu.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI KISUTU**
**DAR ES SALAAM**
**KESI YA MADAI 202 YA MWAKA 2019**

**FAST JET AIR FORCE ONE……………………………MDAI**

**DHIDI YA: ROSELYNE MOLLEL, MANTUMU MOHAMED, ROBBY MAGORI, MONICA DE MELLO, FLAVIANA MSAKI, JACK MGONJA, ENNA LUTENGANO, HALIMA RAJABU, MARIAM SAROGA, MARY SWAI, SANDRA NASORO, ANGELA MOLLEL, SHARIFA MATAKA…………………………WADAIWA**

**KWA: FLAVIANA MSAKI**
**SANDRA NASORO………..POPOTE ULIPO**

**KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa mdai ameleta madai yake ambayo maelezo ya mdai yameelezwa katika nakala ya madai ambazo zinaweza kupatikana katika Mahakama hii, kwa hiyo unahitajiwa kuhudhuria katika Mahakama hii binafsi au kwa Wakili au mwakilishi ambaye anaruhusiwa kisheria, kusikiliza maamuzi ya kesi tajwa hapo ambayo wewe ndiye mdaiwa, siku ya tarehe 30/06/2021 (saa 07:30 Mchana mbele ya Mhe. Y.R. Ruboroga, PRM.

**ANGALIA:** Kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu, Mahakama ikithibitisha kama umepokea kuitwa shaurini, itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 25/06/2021.

116333302

## KUPOTEA KWA CHETI



**TUMPE PHILIP TULO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S 0229-0120** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary **KONDOA** mwaka **2003**,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
**Polisi taarifa DAR/MAG/RB/319553/2021**

116333402

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JAMES FREDERICK MARO**
Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari Toyota RAV4, Yenye namba za usajili T 508 BES
Namba mpya T 729 AJW. Toyota .
Yenye Chassis namba SXA117100602 na Injini namba 3SFE2495106
Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi .
Polisi Taarifa :
**KIL/MOS/RB/310841/2021**

116333902

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**HASSAN ISSA LEMBELY**
anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya **BOXER** yenye namba za usajili **MC 340 ATL.**
Chasis **No.MD2AZIB28DWG76907,** Engine No. **PFZWDG-39203.**Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi:
**DOM/RB/10140/2021.**

116334002

## KUPOTEA KWA CHETI



**IRENE GODFREY MGONGO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S 4733-0041** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary **ST.MARGARET MARIA ALAKOK GIRLS** mwaka 2014,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
**Polisi taarifa DAR/KIG/RB/310566/2021**

116334402

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**PAUL TEGU HAULE**
ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YAKE YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 482 DGV** – TOYOTA **BREVIS**. YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI:
**KAWE/RB/2847/21/21.**

116334302

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**ELIA MESHACK NDALE** anagtangaza kupotelewa na kadi ya pikipikii aina ya GUTA yenye namba za usajili **MC 697 BRR,** yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa **MBE/MBE/RB/310954/2021**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**MBEYA**
**UTHIBITISHO NA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**SHAURI LA MIRATHI NAMBA 2 LA MWAKA 2021**
**MAOMBI YA BARUA YA USIMAMIZI WA MIRTHI YA NEWTON PAMBEYA MWAUPINA KYANDO……………….MAREHEMU**
**NA**
**1. MARIE MANGULA KYANDO**
**2. JANE KYANDO**
**KIUNSI……………………………..WAOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika mirathi ya Marehemu aliyetajwa hapo juu, wanafahamishwa kufika na kuangalia mwenendo wa shauri ili kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa barua za usimamizi wa mirathi kwa waombaji waliotajwa hapo juu. Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya **tarehe 22/07/2021.**
**Imetolewa Mbeya leo tarehe 14/06/2021.**

Z.D. LAIZER
NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
MBEYA

116334502

## NYUMBA INAPANGISHWA

**NYUMBA INAPANGISHWA IPO KAYANGA-KARAGWE KARIBU NA IDARA YA MAJI, SELF CONTAINER INA VYUMBA VIWILI IMEANGALIA KWENYE BARABARA YA LAMI KARAGWE-BUKOBA.BEI ELFU 80,000 KWA MWEZI**

**MAWASILIANI 0778-668182,0620-670166**

***NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA***




TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Joto kali sababu kuondoa amri uvaaji barakoa

**Rome,** ITALIA

ITALIA imeondoa uvaaji barakoa nchi nzima, imetajwa kwamba kitisho ni kidogo, hatua ambayo ni kubwa katika nchi hiyo iliyokuwa ya kwanza kuathirika vibaya zaidi na virusi vya corona, barani Ulaya, Februari mwaka jana.

Kwamba watu hawalazimiki kuvaa barakoa ambako viwango vya joto vinatarajiwa kupanda, kufikia nyuzi joto 40 wiki hii katika maeneo yake ya Kusini.

Hatua hiyo ilianza kutekelezwa jana Jumatatu, wizara ya afya nchini humo, ilisema mikoa yote 20 ya nchi ni salama na kwamba kitisho ni cha chini kwa mujibu wa utaratibu wa mfumo wa taifa wa kupima viwango vya kitisho cha Covid-19.

Giovanni di Perri, Mkurugenzi wa Hospitali ya Magonjwa ya Kuambukiza, alisema maambukizi yamepungua sana nchini humo, sababu mojawapo ikiwa inatokana na watu wengi kuchanjwa. **DW**

# Nyusi apania kuwashinda wanajihadi

**Cabo Delgado,** MSUMBIJI

RAIS wa Msumbiji Filepe Nyusi (pichani), amesema ana matumaini serikali yake itawadhibiti wanajihadi wanaotatiza usalama na kuwaua raia katika mkoa wa wa Cabo Delgado.

Rais Nyusi, akizungumza wakati wa sherehe za 46 za uhuru wa taifa hilo, alisema wanajeshi wa taifa hilo kwa ushirikiano na wale kutoka nje, karibuni watalimaliza shughuli zote za wanajihadi katika mkoa wa Cabo Delgado.



"Operesheni kali ya kuwasaka na kuwatokomeza wanajihadi hao itaendeshwa hivi karibuni kwa usaidizi wa kutosha kutoka kwa mataifa ya SADC na mengine yanayojali usalama wetu," alisema Rais Nyusi.

Juma lililopita viongozi wa mataifa ya SADC, walikubaliana kuwatuma wanajeshi nchini Msumbiji, kulisaidia taifa hilo kutokemeza wanajihadi.

Katika mkutano huo, Rais Nyusi alitoa wito kwa mashirika ya kiraia kuendelea kusaidia raia wa Cabo Delgado, ambao wamekimbia makwao kutokana na shughuli za wanajihadi hao. **RFI**

# Misri, Jordan, Iraq kuimarisha ushirikiano

**Baghdad,** IRAQ

WAKUU wa nchi za Misri, Jordan na Iraq wamefanya mkutano wa kilele na kukubaliana kuimarisha ushirikiano wa kiusalama na kiuchumi.

Rais wa Misri Abdel Fatah al Sisi kwa mara ya kwanza alikwenda Iraq, kushiriki mkutano huo pamoja na Mfalme Abdulla II wa Jordan na viongozi wa Iraq.

**Iraq pia inataka kujionyesha kama msuluhishi kati ya nchi za Kiarabu na Iran...**

Ziara hiyo imekuja wakati nchi hiyo ya Iraq ikitaka kujisogeza karibu na washirika wa Marekani wa nchi za Kiarabu katika Mashariki ya Kati.

Iraq pia inataka kujionyesha kama msuluhishi kati ya nchi za Kiarabu na Iran baada ya kuripotiwa kuandaa mazungumzo mwezi Aprili kati ya Iran na Saudi Arabia.

Rais Al Sisi na Mfalme Abdallah II wa Jordan walikutana na wenyeji wao, Rais Barham Saleh na Waziri Mkuu Mustafa al Kadhemi, Rais wa Iraq alisema ujumbe uliotokana na mkutano wao ulikuwa muhimu katika wakati ambao kuna changamoto nyingi za kikanda.

Aidha, viongozi hao walijadiliana kuhusu suluhisho la kisiasa linalozingatia azimio la Umoja wa Mataifa (UN) katika mgogoro wa Syria. **DW**



Watoto wakicheza katika eneo la maji ikiwa ni mapumziko mjini Vancouver, nchini Canada, juzi. Canada inashuhudia ongezeko la joto lililofikia nyuzi joto 46.6C hadi kufikia jana na kuvunja rekodi ya miongo takribani nane. **PICHA: XINHUA**

# Canada yarekodi joto kupindukia

**Ottawa,** CANADA

CANADA imeandika rekodi baada ya kushuhudia joto kali Magharibi mwa nchi na Pasifiki ya Amerika Kaskazini, ambalo haliwahi kutokea kwa miango kadhaa.

Eneo la Lytton, British-Columbia nchini Canada, joto lilifikia nyuzi joto 46.6C mwishoni mwa wiki na kuvunja rekodi ya miaka 84, maofisa wamesema, jana. Kituo maalum cha kutunza rekodi za joto, kimerekodi joto kali pia kwenye mikoa tofauti.

Marekani na Canada, zimetoa tahadhari kwa raia wake juu ya viwango vya joto vilivyotaja ni hatari na pengine kudumu kwa wiki yote hii.

Wataalamu walisema kwamba mabadiliko ya hali ya hewa yanatarajiwa kuongeza mzunguko wa matukio ya hali ya hewa kali, kama mawimbi ya joto. Ingawa hawajahusianisha hali hiyo maeneo mengine duniani.

Imeshuhudiwa watu kadhaa wakikaa maeneo yenye viyoyozi huku baa na migahawa mingine wakiogelea. **BBC**

# 21 wanyongwa kujihusisha na Al-Shabab

**Puntland,** SOMALIA

WANAUME 21 wameuawa katika Jimbo la Puntland, baada ya kupatikana na hatia ya kuwa wanachama wa kundi la wanamgambo wa Kiislam la al-Shabab.

Walihukumiwa na mahakama ya kijeshi huko Galkayo na kupigwa risasi na kikosi maalum kilichojihami kwa bunduki Redio ya serikali ilisema kuwa 18 kati yao walikuwa wametekeleza mauaji na ulipuaji wa mabomu kwa zaidi ya muongo mmoja.

Hukumu kama hizo za kifo zilikuwa zimetolewa na mahakama katika maeneo mengine ya Somalia hapo awali. Ingwa iliripotiwa kuwa ni idadi kubwa zaidi ya mauaji ya wafuasi wa Al-Shabab kuwahi kutokea Puntland. **BBC**

# FATI AKARIBIA KURUDI UWANJANI




**BARCELONA,** Hispania

RIPOTI za hivi karibuni zinaonyesha kwamba, Ansu Fati anaweza kurudi polepole kwenye msimu ujao na kuanza kucheza, lakini uamuzi wa mwisho utafanywa katika siku zijazo.

Fati anaendelea vizuri tangu afanyiwe operesheni mwezi mmoja na nusu uliopita huko Porto nchini Ureno na anaendelea kuuguza jeraha la goti alilopata Novemba mwaka jana.

Kinda huyo mwenye umri wa miaka 18, kwa sasa anaendelea na matibabu na daktari maalumu mjini Madrid, lakini anawasiliana kila wakati na timu ya matibabu ya Barcelona.

Na hii inaweza kuwa taa kwa mshambuliaji huyo machachari, na ingawa kupona kwake ni polepole, kila kitu kinaenda kulingana na mpango.

Fati bila shaka atalazimika kufanya kazi kwa kasi yake mwenyewe, akiwa nje ya uwanja tangu Novemba 7, mwaka jana lakini anasubiri ruhusa kutoka kwa madaktari.

Bado hajaongeza mkataba na klabu yake hiyo, lakini anafikiriwa kama mmoja wa matarajio mazuri hapo Camp Nou.

Licha ya umri wake, Fati amevunja rekodi nyingi tayari, akiwa mchezaji mwenye umri mdogo zaidi kucheza kikosi cha kwanza cha Barcelona, kufunga kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na LaLiga.

## Hazard, De Bruyne wazusha hofu Ubelgiji



**SEVILLE,** Hispania

EDEN Hazard amezua hofu kwenye kikosi cha Ubelgiji baada ya kuumia goti katika mchezo ambao waliwatoa Ureno hatua ya 16-bora kwenye michuano ya Euro 2020, huku kocha, Roberto Martinez pia akisubiri taarifa ya Kevin De Bruyne.

Ubelgiji walishinda bao 1-0 na kumwondoa Cristiano Ronaldo na Ureno kwenye michuano hiyo na sasa wamefuzu kucheza robo fainali Jumapili, lakini kuna uwezekano mkubwa wakawakosa Hazard na De Bruyne.

Thorgan Hazard alifunga bao kwa shuti kali nje ya 18 na kuwezesha Ubelgiji kufuzu robo fainali na sasa watakutaka na Italia, huku Hazard akitolewa kutokana na kupata majeraha na De Bruyne akaomba kutoka baada ya kuumia kifundo cha mguu.

Na baada ya mchezo huo, Hazard – ambaye amekuwa majeruhi kwa muda mrefu tangu ajiunge na Real Madrid mwaka 2019 – aliwaambia waandishi wa habari: "Nimejiumiza mwenyewe, nahisi maumivu makubwa.

## *De Ligt akubali lawama Uholanzi kutolewa Euro*

**BAKU,** Azerbaijan

MATTHIJS de Ligt amekubalia lawama kutolewa kwa Uholanzi kwenye michuano ya Euro 2020 baada ya kuonyeshwa kadi nyekundu wakati wakifungwa mabao 2-0 na Jamhuri ya Czech hatua ya mtoano ya 16-bora.

Mlinzi huyo wa Juventus, alitolewa nje dakika 10 baada ya kuanza kwa kipindi cha pili baada ya marudio ya VAR kuonyesha akiuzuia mpira kwa mkono na kumfanya Patrik Schick kukosa nafasi ya wazi kufunga bao.

Mabao kutoka kwa Tomas Holes na Schick, likiwa la nne kwenye michuano hiyo, yalikihakikishia kikosi cha kocha, Jaroslav Silhavy kufuzu hatua ya robo fainali ya michuano hiyo ambapo watakutana na Denmark mjini Baku.

Uholanzi hawakuwa kwenye kiwango bora kwenye mchezo huo na kukifanya kikosi hicho cha kocha, Frank de Boer kutopiga shuti hata moja langoni mwa wapinzani wao.

Bado De Ligt akafanya kosa hilo na hivyo kumfanya atolewa nje na sasa amekubali kwamba yeye ndiye chanzo cha timu yake kutolewa.

"Bila shaka tunajisikia vibaya. Kiuhakika tulipoteza mchezo kwa sababu ya kile nilichofanya mimi," alisema akiiambia NOS.

"Sikutakiwa kufanya kile kilichotokea, lakini nakubali lawama kwamba mimi ndiye chanzo cha hayo yote."



HABARI MICHEZO

# Haaland kumrithi Lewandowski Bayern

**MUNICH,** Ujerumani

BAYERN Munich wanamtazama Erling Haaland kuwa mtu mwafaka wa kwenda kurithi mikoba ya Robert Lewandowski kama ataondoka klabuni hapo.

Straika wa Poland, Lewandowski amekuwa akihusishwa na mpango wa kuachana na mabingwa hao wa Bundesliga kwenye dirisha hili la majira ya joto baada ya kudumu kwenye timu hiyo kwa miaka saba.


Na kama Lewandowski ataamua kubaki kwa msimu ujao, basi Bayern watafanya kazi ya kunasa huduma ya Haaland mwakani.

Lewandowski mwenye umri wa miaka 32, ataingia kwenye mwaka wa mwisho wa mkataba wake huko Bayern kwenye dirisha la majira ya joto la mwakani na imeelezwa kuna mazungumzo hafifu sana ya kuongeza mkataba mpya.

Taarifa zinadai kwamba mabosi wa Munich wameamua kukaa kimya juu ya ishu ya Haaland kwa sababu hawataki kumpa presha straika wao namba moja, Lewandowski.

Lakini, Lewandowski ameripotiwa kujiweka mwenyewe kwenye mazingira ya kunaswa na Chelsea kutokana na kile alichosema mwezi uliopita, ambapo staa huyo aliiambia Canal+: "Nimeweka milango wazi. Najisikia vizuri hapa Bayern, jiji ni safi na klabu kubwa.

"Lakini, siku zote nipo kwenye mipango ya kujifunza lugha mpya, utamaduni mpya. Hilo linaweza kutokea sasa au baada ya maisha yangu ya soka, hata mimi bado sifahamu."





# SANCHES ANUKIA ARSENAL

**LONDON,** England

KIUNGO wa timu ya Taifa ya Ureno anayekipiga ndani ya Klabu ya Lille inayoshiriki Ligue 1, Renato Sanches amewekwa kwenye rada za Arsenal na Liverpool za England.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 23, juzi Jumapili alikuwa kwenye kikosi cha Ureno kilichocheza na Ubelgiji hatua ya 16-bora Euro 2020.

Ripoti zinaeleza kwamba, Kocha Mkuu wa Arsenal, Mikel Arteta anamfuatilia kwa karibu nyota huyo ili ajiunge nao msimu ujao katika eneo la kiungo.

Kwenye Euro 2020, alianza mchezo mmoja kikosi cha kwanza huku michezo miwili akitokea benchi na alionyesha kiwango bora kwa timu hiyo jambo ambalo limezivutia timu nyingi.

Arsenal ipo kwenye harakati za kuimarisha kikosi chake kwa ajili ya msimu ujao wa Ligi Kuu England.

Kwa mara ya kwanza msimu huu tangu mwaka 1996, Arsenal haitashiriki kwenye michuano ya Ligi za Ulaya baada ya kumaliza nafasi ya nane kwenye msimamo wa ligi.

# *Benitez kutangazwa kocha mpya Everton*

**LIVERPOOL,** England

RAFAEL Benitez anatarajiwa kutangazwa kama kocha mkuu wa timu ya Everton akichukua nafasi ya Carlo Ancelotti ambaye amerejea Real Madrid ya Hispania.

Ancelotti ametua Madrid kuchukua nafasi ya Zinedine Zidane ambaye alijiuzulu hapo baada ya kumaliza msimu bila taji lolote.

Everton inajulikana kuwa timu ambayo haipendi sana kufanya uchaguzi wa makocha wake kabla ya kuwaajiri, lakini hii inaweza kuwa tofauti mwaka huu ambapo uteuzi wa kocha Benitez unaweza kufanyika rasmi wiki ijayo.

Kocha huyo anajiunga na Everton akitokea DL Pro ya nchini China ambako alikaa huko kwa miaka miwili.

Kabla ya klabu hiyo, Rafa aliwahi kuwa kocha wa Liverpool, Real Madrid na baadaye Newcastle United.



# DONDOO SOKA
## MAGAZET LAYA




# MESSI AKUBALI KUSAINI MKATABA MPYA BARCA

### Kwa sasa mshambuliaji huyo anatarajia kumalizia soka lake hapo Catalunya ambapo...

**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA inajiandaa kutangaza rasmi kwamba, wamefikia makubaliano na Lionel Messi kuhusu mkataba mpya.

Kwa mujibu wa Football Espana na mwandishi wa Sky Sport Italia, Fabrizio Romano, Barcelona wameshafikia makubaliano, na Messi atasaini mkataba mpya ndani ya siku chache zijazo.

Hivyo, Barcelona watatangaza rasmi kufikiwa kwa makubaliano hayo wakati Messi akiwa na timu yake ya Taifa ya Argentina kwenye michuano ya Copa America inayoendelea.

**Mkataba wa Messi na miamba hao wa LaLiga unamalizika mwishoni mwa wiki hii na mshindi huyo mara sita wa Ballon d'Or alikuwa anahusishwa na mpango wa kuondoka.**

Lakini sasa kwa mujibu wa ripoti hiyo, Messi amekubali kuongeza mkataba wa kuendelea kukaa hapo Camp Nou kwa miaka miwili na zaidi.

Nahodha huyo wa Barca alikuwa anahusishwa na miamba ya Ligi Kuu ya England, Manchester City na matajiri wa jiji wa Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, Paris Saint-Germain.

Messi mwenye umri wa miaka 34, sasa anatarajia kumalizia soka lake hapo Barca ambapo amecheza kwa kipindi cha miaka yake yote ya soka.

## ZISIKUPITE

### CITY WAMGEUKIA GRIEZMANN

MANCHESTER City huenda wakamlenga mshambuliaji wa Barcelona na Ufaransa, Antoine Griezmann, 30, kama mbadala wa straika wa England na Tottenham, Harry Kane. ***(Fichajes)***

### WHITE HAJUI CHOCHOTE

MLINZI wa Brighton na England, Ben White, 23, amesema kwamba, hajui kile ambacho ni kweli kuhusu uvumi wa kujiunga na Arsenal kwa dau la pauni milioni 50. ***(TalkSport)***

### LINGARD MIAKA MITATU UTD

MANCHESTER United imempatia, Jesse Lingard mkataba mpya wa miaka mitatu wakati huu kiungo huyo wa England akiwa anawaniwa kusajiliwa moja kwa moja na West Ham alikokuwa anacheza kwa mkopo. ***(Mirror)***

### COMAN AWANIWA LIVERPOOL

LIVERPOOL inawania kumsajili mshambuliaji wa Bayern Munich na Ufaransa, Kingsley Coman, 25 na inawasiliana na wakala wa mchezaji huyo. ***(Sport 1 via Metro)***

### BELLERIN ATAKIWA INTER

KLABU ya Inter Milan imewasiliana na wakala wa beki wa kulia wa Arsenal, Hector Bellerin, 26, huku klabu hiyo ya Italia ikimlenga mchezaji huyo raia wa Hispania ili kuziba nafasi ya Achraf Hakimi. ***(Gianluca di Marzio)***

### XHAKA HUYOOO ROMA

KIUNGO wa kati wa Arsenal na Uswisi, Granit Xhaka, amethibitisha kuondoka katika klabu hiyo ya Ligi Kuu England na kujiunga na AS Roma baada ya michuano ya Euro 2020. ***(90 min)***

### CAMAVINGA RASMI UNITED

KLABU ya Manchester United itakutana na wakala wa kiungo wa kati wa Rennes, Eduardo Camavinga, 18 wiki ijayo kumsainisha mkataba rasmi. ***(RMC, via Mirror)***

### PRAETT KUTUA ARSENAL

MIAKA miwili baada ya kukataa kujiunga na Arsenal, kiungo wa kati wa Leicester na Ubelgiji, Dennis Praett, 27, huenda akasajiliwa na klabu hiyo katika dirisha hili la uhamisho wa kipindi cha majira ya joto. ***(Express)***

### ANDERSON KURUDI LAZIO

KIUNGO wa kati wa West Ham, Felipe Anderson, 28, huenda akarudi Lazio baada ya klabu hiyo kuanzisha mazungumzo ya kumsajili mchezaji huyo. ***(Mail)***

### MADUEKE KUMRITHI SANCHO

BRORUSSIA Dortmund itamlenga mshambuliaji wa PSV Eindhoven na England, Noni Madueke, 19, kuchukua nafasi itakayoachwa wazi na Jadon Sancho ambaye anatarajiwa kutia saini kule Manchester United. ***(Ruhr Nachrichten)***

# KVZ yatangulia nusu fainali FA

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya KVZ imetinga hatua ya nusu fainali ya michuano ya Kombe la Shirikisho Zanzibar (ZFF), maarufu FA Cup, baada ya juzi kuitoa Kundemba kwa mikwaju ya penalti katika mchezo wa robo fainali uliopigwa Uwanja wa Amaan visiwani hapa.

Katika mchezo huo wa robo fainali uliowapa tiketi KVZ ya kutinga nusu fainali, ulifikia changamoto hiyo ya mikwaju ya penalti baada ya timu hizo kumaliza dakika 90 zikiwa zimefungana bao 1-1.

Akizungumza na gazeti hili baada ya mchezo huo, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Sheha Khamis, alisema malengo yake makubwa ni kuhakikisha wanapata nafasi ya kushiriki michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika kwa kutwaa taji hilo FA.

"Sijabweteka, bado nataka kuhakikisha mpaka natetea ubingwa wa FA, wachezaji wetu tumewajenga kisaikolojia wasidharau timu yoyote tunayocheza nayo, kila mchezo uliokuwa mbele yetu basi tuhesabu ni mgumu," alisema.

Timu ya KVZ ndio mabingwa watetezi wa michuano hiyo ambayo bingwa huiwakilisha Zanzibar kwenye Kombe la Shirikisho Afrika.

Mechi nyingine ya hatua hiyo ya robo fainali ilipigwa jana katika Uwanja wa Amaan kwa timu ya Polisi kuvaana na Chuoni.

Kabla ya mechi hiyo, Kocha Mkuu wa Polisi, Yusuf Sape, alimwambia mwandishi wetu kuwa lengo lake msimu huu ni kuhakikisha timu hiyo inatwaa taji hilo ili kupata nafasi ya kuiwakilisha Zanzibar kwenye michuano ya kimataifa.

"Tumejiandaa kupata alama tatu, japo tunajua mchezo utakuwa mgumu, Chuoni ni wazuri tumecheza nao Ligi Kuu Zanzibar, lakini kila timu lengo lake ni kusonga mbele, muhimu ni wachezaji kujituma na kufuata maelekezo ya mwalimu," alisema.

# AZAM YAPANIA KULIPA KISASI SIMBA CHAMAZI

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Azam imesema kuwa inakubali matokeo ya mechi ya nusu fainali ya Kombe la Shirikisho la Soka nchini (TFF), maarufu kama Kombe la FA, ya kuchapwa bao 1-0 dhidi ya Simba katika Uwanja wa Majimaji mjini Songea, lakini imesema italipiza kisasi kwenye mechi ya Ligi Kuu Julai 14, mwaka huu watakapokutana Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Thabit Zacharia 'Zaka za Kazi', amesema wameumia sana na matokeo hayo, lakini wanakwenda kujipanga ili hali kama hiyo isitokee tena, badala yake wanajiandaa kulipiza kisasi kwenye uwanja wao wa nyumbani.

**"Tumekubali kufungwa. Tulipoteza umakini tukafungwa goli mwishoni. Pamoja na hayo tulikuwa na uwezo wa kuimaliza mechi mapema. Kuna nafasi ambazo wachezaji wetu walizipata, Salum Aboubakar, Idd Nado na Mudathir Yahaya, walipata nafasi ambazo zingeweza kumaliza mchezo, lakini hatukuzitumia.**

"Tunarudi nyumbani kujipanga na mechi nyingine dhidi ya Simba Julai 14 kwenye Uwanja wetu, Chamazi, nina uhakika tutalipa kisasi. Itakuwa ni mechi ya kisasi. Pia tunahitaji pointi tatu muhimu kwenye Ligi Kuu ili kujiweka kwenye nafasi nzuri," alisema Zacharia.

Kwenye mechi ya mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu, Simba na Azam zilitoka sare ya mabao 2-2.

Lakini Jumamosi iliyopita kwenye Uwanja wa Majimaji, Simba iliichapa Azam FC bao 1-0 na kutinga hatua ya fainali ambayo itachezwa Julai 25, mwaka huu dhidi ya watani zao wa jadi, Yanga kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika, mjini Kigoma.

Kwa upande wa Yanga, yenyewe imetinga hatua hiyo baada ya kuichapa Biashara United kwa bao 1-0 katika mechi ya nusu fainali iliyopigwa Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi mjini Tabora Ijumaa iliyopita.

## NIPO MAKINI...



Mwanachama na shabiki mkongwe wa Klabu ya Yanga, Juma Ally Mpili maarufu Mzee Mpili, akisikiliza kwa makini wakati mgeni rasmi, Rais wa zamani wa Tanzania, Jakaya Kikwete, akitoa nasaa zake kwa wanachama wa Yanga waliohudhuria kwenye Mkutano Mkuu wa kupitisha mapendekezo ya katiba kuelekea mabadiliko ya uendeshaji wa klabu hiyo, jijini Dar es Salaam juzi. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Biashara yalia na uzoefu kipigo Yanga*

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Biashara United, Patrick Okumu, amesema wametolewa kwenye hatua ya nusu fainali ya Kombe la Shirikisho la Soka nchini (TFF), maarufu Kombe la FA, kutokana na uzoefu tu na si kingine.

Kocha huyo alisema kwenye mechi ya nusu fainali dhidi ya Yanga iliyopigwa Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi mjini Tabora Ijumaa iliyopita, walitawala kila kitu, lakini kutokuwa na wachezaji wazoefu wa kutosha, kuliwaangusha.

Okumu alisema hayo kutokana na kushindwa kichapo cha bao 1-0 dhidi ya Yanga katika mchezo huo.

"Wenzetu walikuwa na wachezaji wa kimataifa na wenye uzoefu kwenye mechi kubwa, ndicho kilichokuwa tofauti kati yetu. Lakini kwenye soka sisi tulikuwa vizuri zaidi, hasa kipindi cha pili, tukawashambulia kwa muda mrefu, lakini tukashindwa," alisema kocha huyo raia wa Kenya.

Hata hivyo, amekisifu kikosi chake kwa kupambana kwenye mechi dhidi Yanga, lakini kufika hatua hiyo kwani timu nyingi ambazo ni kubwa na zenye majina makubwa zaidi ya Biashara United, hazikufanikiwa kugusa.

"Kwa sasa nakwenda kufanya maboresho kutokana na makosa niliyoyaona kwenye mechi yetu na Yanga. Narudi kwenye ligi na nina nafasi nzuri ya kucheza mechi za kimataifa msimu ujao, kama nitaweza kushinda mechi moja tu kati ya mbili nilizonazo," alisema.

Biashara United ambayo ipo nafasi ya nne kwenye msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na pointi 49 baada ya kushuka dimbani mara 32, kama ikimaliza katika nafasi hiyo itaiwakilisha nchi kwenye Kombe la Shirikisho Afrika.

# Michezo

Jumanne Juni 29, 2021

Nipashe




Messi akubali kusaini Barca UKURASA 22

JUU KWA JUU...



Mshambuliaji wa Ureno, Cristiano Ronaldo (kushoto), akiwania kumiliki mpira juu kwa juu na beki wa Ubelgiji, Jan Vertonghen, katika mechi ya hatua ya 16-bora ya michuano ya Euro 2020 iliyopigwa Uwanja wa Estadio La Cartuja de Sevilla, Hispania juzi na Ubelgiji kushinda bao 1-0. **PICHA: MTANDAO**

# Gomes, Nabi waliamsha mtifuano Simba, Yanga

●●● Akataa kuwa daraja la ubingwa, Mfaransa asema hakuna namna, tiketi 'kiduchu' zaanza kuuzwa...

**Na Saada Akida**

WAKATI homa ya pambano la watani wa jadi, Simba na Yanga likizidi kupanda, makocha wa timu hizo wameviwaisha mapema vikosi vyao kambini huku kila mmoja akitamba kuibuka na ushindi katika mechi hiyo ya Ligi Kuu Bara itakayopigwa Jumamosi kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

**Simba ambao watakuwa wenyeji wa mechi hiyo ya mzunguko wa pili, wameingia rasmi kambini leo huku Yanga wakiingia jana tayari kwa ajili ya kujiandaa na mechi hiyo.**

Makocha hao wakizungumza na gazeti hili kwa nyakati tofauti jana, kila mmoja alitamba kuibuka na ushindi Jumamosi ambapo Kocha Mkuu wa Simba, Didier Gomes, alisema mechi hiyo kwao ni fainali na anahitaji kuimarisha zaidi kikosi chake ili kuibuka na ushindi.

"Katika soka lolote linaweza kutokea, vijana wangu wako imara, tunatakiwa kupambana kuhakikisha tunatangaza ubingwa katika mchezo huo ambao utakuwa wa ushindani mkubwa.

"Bado tuna nafasi ya kufanya vizuri na nina waamini wachezaji wangu kufanya yale ya mazoezini, tutazidi kupambana ili kuwa imara wakati wote," alisema Gomes huku akieleza kwamba mshambuliaji Chris Mugalu ambaye alikuwa majeruhi amerejea na tayari ameanza programu maalum.

Kwa upande wa Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, alisema wameingia kambini kujiandaa na mechi hiyo, lakini wataitumia kujiwinda na mchezo wa fainali wa Kombe la FA dhidi ya Simba.

"Ni mechi ngumu na ushindani mkubwa kwa sababu kila mmoja wetu tunahitaji matokeo, kwetu ni lazima tushinde mechi hii kwa sababu bado tuko katika mbio za ubingwa na hatutaki kuwa daraja la wapinzani wetu kutangaza ubingwa kupitia mchezo huo," alisema kocha huyo.

Kwa upande wa kamati ya ulinzi na usalama kwa kushirikiana na serikali kupitia Wizara ya Michezo, Bodi ya Ligi na wahusika wa Klabu za Simba na Yanga jana, wamekutana na kujadili maandalizi ya mchezo huo.

Mkurugenzi wa Maendeleo ya Michezo nchini, Yusuph Singo, alisema: "Kila kitu kimeenda vizuri kuhusu maandalizi ya mchezo huo utakaopigwa Jumamosi, kwa upande wa usalama uko vizuri na tumejipanga kuhakikisha mashabiki wanakuja na kuondoka salama."

Kuhusu baadhi ya mashabiki ambao walikata tiketi awali, lakini hawajarejeshewa, Meneja wa N-Card, Nasra Mugheiry, alisema walionunua tiketi katika mchezo uliopita wanatakiwa kwenda na kadi zao ili kuhakiki miamala yao na kisha kuruhusiwa kuingia uwanjani.

"Tiketi zimeanza kuuzwa leo (jana) kupitia katika mitandao ya simu na leo, tutaanza kuuza katika vituo, ikiwamo Klabu ya Simba, Yanga, Vunjabei Sinza na TFF," alisema Nasra.

Alisema kwa upande viti vya mzunguko zimebaki nafasi 2,218 kwa ambapo tiketi ni Sh. 7,000 na viti vya rangi ya machungwa ni 11,280 kwa Sh.10,000, VIP B zimebaki nafasi 284 kwa Sh. 20,000 huku VIP A na C zikiwa zimejaa.

# Kelvin John anga moja na Grealish

**Na Mwandishi Wetu**

MSHAMBULIAJI wa kimataifa wa Tanzania, Kelvin John, aliyesajiliwa na Klabu ya KRC Genk, ameingia anga moja na wachezaji nyota wa Chelsea, Manchester United na Aston Villa, imefahamika.

Kelvin, 18, kwa sasa ni mmoja kati ya wachezaji ambao wapo chini ya Kampuni ya wakala, ICM Stellar Sports, ambayo ni wakala wa kiungo wa Aston Villa, Jack Grealish, Luke Shaw wa Manchester United pamoja na Mason Mount na Ben Chilwell wanaochezea Chelsea.

Mshambuliaji huyo chipukizi wa kimataifa wa Tanzania, wiki iliyopita alijiunga na KRC Genk ya Ubelgiji baada ya kusaini mkataba utakaomalizika mwaka 2024.

Kelvin amejiunga na KRC Genk akitokea akademi ya Brook House Collage ya England aliyojiunga nayo tangu mwaka 2019 baada ya kung'ara kwenye Fainali za Vijana Afrika chini ya umri wa miaka 17.

Genk inamchukulia Kelvin kama Mbwana Samatta ajaye, ambaye aliitumikia klabu hiyo kwa mafanikio makubwa kabla ya kutimkia Aston Villa na baadaye kutolewa kwa mkopo Fenerbahce ya Uturuki.

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042